

# *YESU KRISTO YEYE YULE*

## *JANA, LEO, NA HATA MILELE*



Asante, bwana.

<sup>2</sup> Ni vizuri sana kuwa hapa tena alasiri ya leo, baada ya kuwa na wakati mzuri sana asubuhi ya leo katika kushiriki kwenye Neno la Bwana. Tuna furaha kuwatemebelea tena ninyi watu wazuri hapa katika—katika nyanda hizi.

<sup>3</sup> Na asubuhi ya leo tulikuwa tukizungumza juu ya somo la mafanikio, na *Njia ya Mungu Iliyoandaliwa*. Nami nilikuwa nikiwaambia wale waliokuwa darasani asubuhi ya leo, kwamba watu wanajaribu kujifanikishia kitu fulani wenyewe, daima, kitu ambacho wanaweza kusema, “Nilifanya *hiki*,” ama, “Nilifanya *kile*.”

<sup>4</sup> Nasi tulikuwa tukizungumza juu ya somo la jinsi zingekuwa za ajabu, jinsi habari zingevuma kote ulimwenguni katika dakika chache, kama watu wangeweza kupata njia ya kuidhibiti mvua, kuimwigilia mimea ama kuiondoa kwenye mimea; ama jinsi ambavyo kama wangeweza kupata dawa mahali fulani, ingemfanya mzee kurudia ujana, na mwanamke aurudie ujana, na kuishi milele, mbona, wange—wangepeleka habari kila mahali. Wanajaribu kufanikisha hilo, bali tayari limefanikishwa. Kristo amefanya hili kwa ajili yetu. Naye ni Mafanikio ya Mungu kwa ajili yetu, nasi hatuna budi kumwamini.

<sup>5</sup> Sasa, ibada hizi hazipaswi kuwa...Wakati mwingine zinaitwa ibada za uponyaji wa Kiungu. Sasa, siamini ya kwamba kuna mtu yejote anayeweza kuwaponya watu. Ninaamini ya kwamba uponyaji unafanya kwa imani katika Kristo, kama vile wokovu. Hakuna mtu angaliweza kutusamehe dhambi zetu. Tayari zimesamehewa. Kristo aliokoa ulimwengu na dhambi wakati alipokufa pale Kalvari. Hautakufaa kamwe isipokuwa uuopokee kama faida yako binafsi. Na hivyo ndivyo ilivyo kwa uponyaji. Yote ambayo Mungu angeweza kuwafanyia wagonjwa na wanaoteseka, aliyafanya alipokufa pale Kalvari. Na sasa, Yeye alitununulia hayo, hayo yalikuwa ni mafanikio Yake, sasa, bali kuupokea, inatubidi kuukubali kama mali yetu binafsi, wokovu.

<sup>6</sup> Huenda nikauliza leo, “Ni wangapi wenu ninyi watu mliokolewa miaka kumi iliyopita?” Mikono mingi ingeinuliwa. “Ni wangapi waliokolewa mwaka uliopita?” Mikono ingeinuliwa. Lakini mnaona, hukuokolewa miaka kumi iliyopita, ama mwaka uliopita, uliokolewa miaka elfu moja

mia tisa iliyopita, uliukubali miaka kumi iliyopita, ama—ama wakati wowote ulipoukubali.

<sup>7</sup> Sasa, tayari ni kazi iliyomalizika. Biblia ilisema, “Alijeruhija kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Mnaona? Ni wakati uliopita, jambo ambalo limefanywa. Rahisi sana, na hata hivyo uponyaji wa Kiungu ni mojawapo ya vimeo vikuu vya Biblia, vile vimeo vya Mungu viliyyotolewa kwa Kanisa la Kikristo, ambavyo vimesahaulika muda mrefu, mrefu sana uliopita. Lakini ni kitu ambacho ni mali yetu, ni kitu fulani, ni mali yako binafsi.

<sup>8</sup> Na sasa, kusema kwamba sivyo ilivyo, wamechelewa sana kwa jambo hilo. Lakini nimesafiri yapata mara saba kote ulimwenguni, nami nimeliona jambo hilo katika kila taifa, makumi ya maelfu ya vipofu, viziwi, bubu, wanaoteseka, kansa, uvimbe, ukoma, na hata waliokufa, na taarifa za daktari zimeandikwa, walikuwa wamekufa kwa saa kadhaa, halafu wakafufuliwa tena. Kwa hiyo sasa hayo hayawezi kuwa ni matamshi tu, tusingeyakubali namna hiyo, daktari hana budi kusema hivyo, mnaona. Haina budi kuwa ni taarifa ya kweli kabla hatujaichapisha.

<sup>9</sup> Na kuna makumi ya maelfu ambayo hayajawahi kuchapishwa, kwa sababu mimi sipendi sana kuchapisha mambo, isipokuwa iwe ni mionganii mwetu. Yesu alisema mahali pamoja, “Usimwambie mtu yeyote habari zake. Endeleeni mbele tu na kumpa Mungu utukufu.” Kwa hiyo nafikiri leo hii, tunatilia mkazo sana uchapishaji na kitu ambacho ni cha kujionyesha.

<sup>10</sup> Lakini Kristo si kujionyesha, Yeye ni Mwana wa Mungu, mnyenyeketu. Watu wanawezaje kuamini isipokuwa walichaguliwa kuamini? Kulikuwa na watu wengi katika siku Zake ambaa hawakuamini, bali Yeye aliwijia wale walolihamini.

<sup>11</sup> Wakati fulani uliopita mtu fulani aliniambia... nilikuwa nikisoma makala fulani, na kusema ninii... kuhusu mtoto mchanga huko Mexico ambaye alikuwa amefia mkutanoni, ama, alikuifa asubuhi hiyo yapata saa tatu, na hii ilikuwa saa tano usiku huo, naye daktari akatia sahihi taarifa kwamba alimtangaza mtoto huyo amekufa saa tatu asubuhi hiyo, na saa tano usiku huo alikuwa hai. Nilimwombea pale, baada ya kuona ono, ndipo nikaomba na kumwekeea mikono mtoto huyo mchanga hapo mbele ya karibu, loo, watu hamsini, ama sabini na tano elfu, ndipo maskini mtoto huyo mchanga akaanza kurusha mateke na kupiga mayowe, kisha akafufuka, naye yu hai leo, nijuavyo mimi. Daktari alitia sahihi taarifa yake.

<sup>12</sup> Na kwa hiyo hiyo ni kama mara tano ambapo nimeona jambo hilo likifanyika. Na kwa hiyo mtu huyo akaniambia, “Nitalichunguza hili nione kama hiyo ni kweli.”

Nikasema, “Nitakuepusha na usumbufu huo, hii *hapa* taarifa ya daktari.”

<sup>13</sup> Akasema, “Kama—kama ungeweza kuwafufua, kama—kama ukienda na kuwaombea maelfu nao wangefufuka kutoka kwa wafu, ama, na kansa,” akasema, “bado siamini.”

<sup>14</sup> Nikasema, “Bila shaka huwezi, si kwa ajili ya wasioamini, ni kwa ajili ya wale tu wanaoamini.” Hiyo—hiyo ni kweli, sivyo? Kweli. Yeye anaweza tu kuwashughulikia wale wanaoamini.

<sup>15</sup> Na kuna moja tu, kutokuamini, hebu tuweke hilo niani mwetu, kuna dhambi moja tu. Sasa kunywa pombe, kucheza kamari, kufanya uzinzi, kutumia lughha chafu, hayo si dhambi, hayo ni matokeo ya kutokuamini. Yesu alisema, “Yeye asiyeamini amekwisha kuhukumiwa.”

<sup>16</sup> Katika siku za Bwana wetu, alikuta watu wengi walioishi maisha matakatifu, safi, waungwana wenye heshima, nao walikuwa ni wasomi, vipeo vya elimu. Na hata hivyo, Yeye aliwaambia, “Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi,” kwa sababu hawakumwamini. Mnaona? Ule Ujumbe, hawakuuamini, ambalo liliwfanya wasioamini. Asingeweza kuwasaidia. Katika nchi Yake mwenyewe kulikuwako na wengi asingeweza kuwasaidia, kwa sababu ya kutokuamini. Kwa hiyo asingeweza kukuokoa katika kutokuamini, wala hawezi kukuponya katika kutokuamini. Wewe... Ni—ni rahisi tu kama, “Amini tu.”

<sup>17</sup> Sasa, kabla hujaweza kuamini chochote inakubidi kuwa na namna fulani ya dhana ya kile unachoamini, na ni kwa nini. Siamini ya kwamba Mungu huwaponya watu kusudi tu aonyeshe nguvu Žake za kuponya. Ninaamini Yeye huwaponya watu kuonyesha ya kwamba Yeye hutimiza Neno Lake na kutimiza ahadi Zake. Wakati alipokuja duniani mara ya kwanza, alisema ya kwamba alifanya hivi, “ili litimie neno lilionenwa na nabii.” Neno lote la Mungu halina budi kutimia, lote.

<sup>18</sup> Wakati Yesu alipokufa pale Kalvari, tunajua Nafsi Yake ilienda kuzimuni, mwili Wake ukaenda kaburini, Roho Yake ikaenda kwa Mungu. Pale Kalvari Yeye alisema, “Mikononi Mwako naiweka Roho Yangu.” Ndipo Roho Yake ikaenda kwa Mungu, Baba, mikononi Mwake.

<sup>19</sup> Biblia ilisema Nafsi Yake, Yeye alienda kuzimuni na kuwahubiri wa—wa—wale, waliokuwa kifungoni, ambao hawakutubu katika uvumilivu wa siku za Nuhu.

<sup>20</sup> Mwili wake, tunajua, waliuweka kaburini na kuufungia kwa—kwa mwamba, jiwe kubwa lilifingirishwa, na kutiwa muhuri. Basi, Yesu Mwenyewe, Roho Yake, ambayo kila mmoja wenu anayo, hiyo ilikuwa ni Roho ya Mungu ndani Yake, lakini nyuma ya kizuizi, namna *hii*, Neno la Mungu likingojea kutimizwa. Asingeweza kufufuka mpaka siku ya tatu, kwa sababu Daudi alikuwa amesema, “Sitäiacha nafsi Yake katika kuzimu, wala sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu.”

Sote tunajua ya kwamba uharibifu huingia katika mwili wa mwanadamu katika saa sabini na mbili.

<sup>21</sup> Sasa, Yeye alijua, wakati fulani katika saa hizo sabini na mbili, ya kwamba hana budi kufufuka katika wafu, kwa kuwa aliwaambia, "Uharibuni mwili huu, nitaufufua tena katika siku tatu." Mnaona? "Ubomoeni . . . liharibuni hekalu hili, nitalisimamisha, nitalisimamisha katika siku tatu."

<sup>22</sup> Sasa mnaona, kushikilia na kulitimiza Neno la Mungu, Yeye alikuwa nyuma ya Neno la Mungu akiwa na ahadi mpaka siku tatu kamili zilipotimia. Baada ya siku ya tatu, ukuta ulibomolewa, kwenye asubuhi hiyo, wakati huo ulipotimia, Roho Yake ikishuka kutoka kwa Mungu, ikashuka kaburini, ikaufufua mwili Wake, ikavunja mihuri ya mauti, kuzimu, na kaburi, kisha akafufuka akiwa hai milele.

<sup>23</sup> Sasa, Yeye yu hai leo, Nafsi, mwili, na Roho, Yeye yu hai. Hicho ndicho kiini cha mikutano yetu, daima, ni "Yesu Kristo, ye ye yule jana, leo, na hata milele."

<sup>24</sup> Sasa, kwa msingi wa hili, nami nisingetaka mtu ye yote aseme, "Ndugu Branham, mponyaji wa Kiungu," kwa sababu siamini kuna kitu kama hicho, ninaamini ya kwamba Kristo ndiye Mponyaji, nami ninaamini ya kwamba ametuponya, "Kwa kupigwa kwake sisi tuliponywa."

<sup>25</sup> Na mara nyingi, hapana shaka tuna mchanganyiko hapa katika kanisa hili dogo alasiri ya leo, labda wa madhehebu yote mbalimbali, baadhi yake, ama, madhehebu mengi mbalimbali, nilipaswa kusema, mengi yake, labda, wamefundishwa dhidi ya uponyaji wa Kiungu. Na mara nyingi watu wanaofundisha dhidi yake, bila kujua wanaloafanya, hata hivyo, wameninii, wanachukua dhana mbaya, kwa sababu umewakilishwa vibaya. Wakati mwingine ukweli unaweza kuelezewa vibaya na ukweli kabisa kuharibiwa.

<sup>26</sup> Lakini uponyaji wa Kiungu ni sahihi, ni Neno la Mungu. Kwa hiyo basi, hatuna budi kuweka imani yetu juu ya Neno Lake. Mnaona? Sasa, kuna, na halafu, ni jambo ambalo limefanywa, jambo ambalo Kristo tayari ametufanyia.

<sup>27</sup> Sasa, kumbukeni, tunaamini hili: kwamba Neno la Mungu halina budi kutimizwa; kwamba ni, Mungu Mwenyewe hana kikomo; Yeye hawesi kukosea; Yeye yuko kila mahali, anajua yote, ana nguvu zote, wala hana kikomo; kama sivyo alivyo, basi Yeye si Mungu; na kama Yeye yuko *hivyo*, basi Yeye alijua mwisho tangu mwanzo. Kabla hapajakuwapo na ulimwengu, Yeye alijua tungekusanyika hapa alasiri ya leo, kama Yeye hana kikomo. Yeye alijua kile unachowazia moyoni mwako, kabla ulimwengu haujaanza, alijua kile ungekuwa unawazia wakati huu. Alijua kila mbu ambaye angekuwa duniani, kila wakati angepepesa macho yake. Hiyo ndiyo maana ya asiye na kikomo.

<sup>28</sup> Na kama Yeye si asiye na kikomo, basi Yeye si Mungu. Mnaona? Kwa hiyo hatuna budi kukumbuka ya kwamba hatushughulikii kitu katika—katika wakati na anga kama tulivyo *sisi*, wenye kikomo, tunashughulika na Kitu ambacho hakina kikomo. Na kama Hili ni Neno la Mungu, basi halina kikomo kama vile Mungu asivyo na kikomo. Mnaona? Haya basi. Huna budi kuwa na imani katika Neno, hivyo ndivyo tu litakavyofanya kazi.

<sup>29</sup> Nalo Neno la Mungu ni Mbegu. Nanyi wakulima hapa, mnajua kama ukiweka mbegu ardhini na kuitunza vizuri, kama iko kwenye udongo mzuri, itazaa kile mbegu ilicho. Nalo Neno la Mungu ni Mbegu, na kama ukilitia kwenye udongo mzuri wa imani, na kulitunza vizuri, litazaa kile tu lilicho. Kama ni kwa ajili ya uponyaji, litaleta uponyaji; wokovu, wokovu; furaha, furaha. Na kila ahadi katika Biblia ni kweli.

<sup>30</sup> Basi kumbukeni tu, mnaweza kunishuhudia jambo hili, kwamba mtazamo mzuri wa kiakili kwa ahadi yoyote ya Kiungu ya Mungu utaitimiza, kama unaweza kuchukua msimamo sahihi kwa ahadi hiyo.

<sup>31</sup> Sasa, Biblia ilisema, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu.” Basi kama Neno *lilikwa* ni Mungu, basi *lingali* ni Mungu.

<sup>32</sup> Sasa, hakuna mtu aliye bora kuliko neno lake. Kama huwezi kuliami neno langu, basi ka—kamwe singekuwa ninii... nisingeweza kuwa rafiki yako. Na kama nisingeweza kuliamini neno lako, nisingeweza kukuamini. Lakini wakati tunapoweza kuaminiana, kwa kutuamini! Sasa, hivyo ndivyo unavyomfanya Mungu.

<sup>33</sup> Wala hakuna mtu aliye bora kuliko neno lake. Kama ukitoa ahadi, unapaswa kuitimiza sikuzote, ama useme sababu ya kutoweza, wajulishe, kwa sababu mwanadamu hufungwa na neno lake.

<sup>34</sup> Na Neno la Mungu ndilo Kifungo Chake. Kama Mungu hatimizi Neno Lake, basi si Neno la Mungu. Lakini kama Yeye hutimiza Neno Lake, basi Yeye ni Mungu katika Neno Lake. Mungu angali katika Neno Lake. Na wakati Neno Lake linapoingia ndani yako, basi neno lako linakuwa Neno Lake, hilo ndilo linalolifanya litimie, lolote uliloomba. Rahisi tu namna hiyo.

<sup>35</sup> Mungu ni Muumba. Mungu aliumba kila kitu. Vitu vyote vyema hutoka kwa Mungu; navyo vitu vibaya, vitu viovu, ni kitu kizuri kilichopotoshwa.

<sup>36</sup> Sasa, Shetani hawezি kuumba, kwa hiyo, Shetani hawezি kuponya. Wala hakuna dawa ulimwenguni inayoweza kukuponya. Hakuna daktari atakayekwambia ya kwamba ana dawa itakayokuponya.

<sup>37</sup> Na huenda nikasema hivi: Hatuwapingi madaktari. Tunashukuru kwa ajili ya madaktari na kwa ajili ya dawa zao. Lakini tunaishi katika siku ambapo tuna madaktari bora sana tuliwahi kuwa nao, dawa bora sana tuliyowahi kuwa nayo, hospitali bora sana tulizowahi kuwa nazo, na magonjwa mengi kuliko tuliyowahi kuwa nayo, kwa sababu tuna kutokuamini kwangi kuliko tulikopata kuwa nako. Hiyo ni ninii tu—ndio hadithi yake.

<sup>38</sup> Nimehojiwa na Johns Hopkins, Mayo Brothers; mnajua jinsi huduma kama hii inavyoenenda. Basi Jimmy Mayo na hao wengine, wakasema, "Hatudai kuwa waponyaji, Ndugu Branham, tunakiri kuyasaidia maumbile. Kuna Mponyaji mmoja, huyo ni Mungu," kasema, "tunaweza kung'oa jino, lakini ni nani atakayeponya mahali lilipotoka? Tunaweza kuondoa kidole tumbo, lakini ni nani aponyaye? Kitu fulani hakina budi kuumba."

<sup>39</sup> Hapa, kama nikiukata mkono wangu alasiri ya leo, basi, hatuna dawa katika sayansi yote ya tiba ya kutibu jeraha hilo la kisu mkononi mwangu, hata moja. "Mbona," unasema, "naam, tunayo, Ndugu Branham."

Naomba uniambie ni nini. Naam, bwana. Watu wengi hufa kwa majeraha ya visu. Mnaona? Niambie uponyaji ni nini.

"Vema," ungesema, "Vema, walitia penisilini ndani yake."

Penisilini haiponyi, husafisha tu huku Mungu akiponya.

"Vema," unasema, "vema . . ."

Kis. . . dawa yoyote, inayoweza kuponya jeraha mkononi mwangu, ingeponya jeraha la kisu kwenye koti langu, ingeponya jeraha la kisu kwenye dawati hili.

"Vema," ungesema, "Ndugu Branham, dawa haikutengenezwa kwa ajili ya koti lako wala dawati lako, ilitengenezwa kwa ajili ya mwili wako."

<sup>40</sup> Vema, labda basi, ningekata mkono wangu alasiri ya leo na kuanguka chini nife. Nanyi mnipeleke hapa chini kwenye chumba cha maiti, na, kwenye kituo cha mzishi, na huko wangeupaka mwili wangu dawa usioze, inifanye nionekane wa kawaida kwa miaka hamsini. Mnidunge sindano ya penisilini kila siku. Madaktari walio bora sana waje kutoka Uingereza, Ujeruman, popote wawezapo, na kunitibu kwa miaka hamsini. Jeraha hilo la kisu litakuwa kama tu vile lilivyokatwa siku ya kwanza kabisa.

<sup>41</sup> Sasa, kama dawa imetengenezwa kuuponya mwili wa mwanadamu, kwa nini haiuponyi? Mnaona? Basi dawa haikutengenezwa kuuponya mwili wa mwanadamu wala chochote kile.

<sup>42</sup> Sasa, mnasema, "Vema, Ndugu Branham, uhai umetoka mwilini mwako." Sasa, tumeshika njia. Sasa, mponyaji ni yupi

basi, dawa au uhai? Basi niambieni uhai ni nini, nitawaonyesha Mungu ni nini, mnaona, kwa sababu Mungu ni Uzima. Mnaona? Dawa haifanyizi seli.

<sup>43</sup> Kama nilivunjika mkono wangu, huku nje nikilitengeneza gari langu, nami nikakimbia hapa chini kwa daktari, ambalo lingekuwa ndilo jambo bora kufanya, na kusema, sasa, lakini hili halingekuwa la kimantiki: Ningesema, “Daktari, aisee, niponye mkono wangu upesi sana, bwana, sina budi kumalizia gari langu alasiri ya leo.”

Angeniangalia na kusema, “Ati ulisema nini, Bw. Branham?”

“Uponye mkono wangu, bwana. Wewe ni mponyaji, sivyo? Uponye mkono wangu ili nipate kutengeneza gari langu.”

Mbona, angesema, “Unahitaji uponyaji wa akili.” Na hiyo ingekeuwa ni kweli. Mnaona?

<sup>44</sup> Asingeweza kuuponya mkono wangu, bali angeweza kuuweka mahali ambapo Mungu angeweza kuuponya. Hawezi kutengeneza kalisi na—na uhai kuunganisha mfupa huo pamoja. Kwa hiyo, daktari, pamoja na ufahamu wake, anauweka mfupa mahali pake, lakini Mungu ndiye anayeponya. Mnaona?

<sup>45</sup> Zaburi 103:3, alisema, “Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana, wala usizisahau fadhili Zake zote: Akusameheaye maovu yako yote, akuponyaye magonjwa yako yote.” Kwa hiyo Neno la Mungu haliwezi kushindwa kamwe. Mungu ndiye Mponyaji, huna budi...hatuna budi kukumbuka hilo daima, Mungu ndiye Mponyaji.

<sup>46</sup> Na sasa kwetu sisi katika saa hii, kabla tu ya kuja kwake Bwana wetu Yesu... Na kama vile nilivyosema asubuhi ya leo, kusudi langu hapa lilikuwa ni likizo ndogo. Baadhi ya hawa ndugu watanipeleka hapa juu niende kuvua samaki baada ya ibada kwisha, na niende kuwinda. Nimekuwa hudumani miezi sita sasa, bila kupumzika. Nimedhoofika, nimechoka. Na labda sasa, mara moja, nitaondoka kwenda ng'ambo tena.

<sup>47</sup> Na sasa, nikipitia hapa, baada ya kuwatemebelea mara moja, nilifikiri isingekuwa vema kulipita kundi hili zuri la watu hapa na kutojaribu kumheshimu Bwana wetu, na kufurahia ushirika wenu, na kufanya tuwezacho kuweka mambo yetu pamoja kumtazama Bwana wetu Yesu tena katikati yetu. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu niko hapa kwa siku hizi tatu usiku, ama, siku tatu, ni kushiriki pamoja nanyi karibu na Kristo, na pamoja na ndugu zangu hapa, kuhusu mambo ya Kristo. Na sasa, linaweza kuwa ni jambo kubwa kutukia hapa kama tutaweka tu nia zetu kwenye Neno la Mungu na ahadi ya Mungu. Tuwe na imani.

<sup>48</sup> Ninyi wanaume hapa, mliooa, kwa nini mkawaoa wake zenu? Ulikuwa na matumaini na imani ya kwamba angekuwa mke halisi na mama, na kadhalika. Wanawake, tukirudi kwa waume zenu, ni vivyo hivyo. Wapenzi wanawazia juu ya

ndoaa, unamchunguza mtu utakayeona naye, ama msichana utakayemwoa. Hamna budi kuwaamini, la sivyo afadhali msiwaoe. Mnaona?

<sup>49</sup> Vema, hivyo ndivyo ilivyo kuhusu Kristo. Tuko hapa tukisoma, nasi hatuna budi kuamini kile tunachofuatilia, kwa sababu kumbukeni, baraka zote za ukombozi tayari zimenunuliwa. Tunaweza kuamini hilo kwa moyo wetu wote? kwamba baraka zote za ukombozi zilinunuliwa, Mungu alifanikisha hilo kwa ajili yetu kupitia Kalvari, pamoja na Yesu Kristo.

<sup>50</sup> Yesu alimwambia Baba, “Imekwisha.” Ni nini imekwisha? Mpango wote wa wokovu, kila kitu kimekwisha, “ahadi zote nilizotoa,” a—amaana imewekwa mbele za Mungu, kwamba dhambi zote zimesamehewa, nasi tumerudi kutoka kwenye soko la watumwa, na wote wamekombolewa. “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa uovu wetu, adhabu ya amani yetu, juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Yote yamekwisha.

<sup>51</sup> Sasa, ninataka kulikaribia Neno kwa dakika chache. Na kabla hatujafanya hivyo, hebu na tumkaribie Mwandishi wa Neno, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa ajili ya maombi.

<sup>52</sup> Baba Mtakatifu Mwenye Neema na Mtukufu sana, Mungu Mwenyezi, aliyemfufua tena, Bwana Yesu katika wafu, akamfufua, na amemwasilisha kwetu, mwenye Uhai, Mwana wa Mungu, na kwa miaka elfu moja mia tisa, ametembea pamoja na watu Wake duniani, tuna furaha sana leo, katika wakati huu mkuu wa msiba tunapoambiwa kwamba wamepata, kutokana na utafiti, makombora ambayo yatailipua dunia vipandevipande, na karibu kila taifa linayo, tukijua ya kwamba hilo linalingana kabisa na Neno la Mungu kwa ajili ya siku hizi za mwisho. Ndipo tunaona ninii... mambo hayo, na mataifa, mataifa yenyehambini, mataifa yasiyomcha Mungu yana silaha hiszo, karibu wakati wowote kunaweza kutokea mlipuko, au katika rada kunaweza kuonekana makombora yakitoka katika taifa fulani, ndipo wote wataachilia makombora yao. Ulimwengu usingeweza kuyastahimili.

<sup>53</sup> Basi tunajua hilo lingeweza kutukia kabla ya asubuhi. Lakini kabla haya hayajatukia, tunaambiwa ya kwamba Yesu atakuja kuwapokea watu Wake, kwa kuwa Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu...” Kabla tu ya maangamizi ya ulimwengu, Nuhu alilingia katika safina, kabla ya mvua kunyesha.

<sup>54</sup> Na kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, Malaika alisema, “Hima, njoo upesi, toka hapa, kwa maana siwezi kufanya neno lolote hata utakapotoka hapa.” Basi Lutu akatoka Sodoma, ndipo basi Moto ukashuka, nayo Sodoma ikaangamizwa kabissa, na leo hii iko chini ya Bahari ya Chumvi. Naye Yesu alisema,

“Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu na katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

<sup>55</sup> Halafu basi, kama tunaweza kuona (Nayo sayansi inasema kwamba ni dakika tatu ifike usiku wa manane.) kwamba ulimwengu hauwezi kuyastahimili majira haya yanayotukabili, nasi tunajua lingeweza kutukia wakati wowote, basi kuja kwa Bwana wetu kumekaribia jinsi gani?

<sup>56</sup> Ee Mungu, ibada hizi tatu zinazokuja, tunaomba ya kwamba utatikisa maskini uwanda huu mpana jinsi ambavyo haujawahi kutikiswa hapo kabla. Jalia kwamba kila kanisa litakuwa na uamsho, hapa kupitia humu uwandani, wengi wa hawa watu wa thamani, hawa Waskandinavia na kadhalika, huko nje kwenye nyanda hizi hapa, wataletwa kwa Kristo, ili kwamba wakati Yesu atakapoonekana, kwamba makaburi yatafunguka nasi tutatoka, na kuingia kukutana na Yeye, na kuwa pamoja Naye milele, kwa kuwa tuna nini zaidi duniani cha kutazamia, ila kuja Kwake?

<sup>57</sup> Sasa, Baba, tunajikabidhi Kwako alasiri ya leo, na kusanyiko hili, tubariki pamoja, na jalia ushirika uwe mkuu katika Neno la Mungu.

<sup>58</sup> Ndipo ibada itakapokwisha, nasi tusimame kuomba baraka, kisha twende katika makazi yetu mbalimbali, wengine huko nje uwandani, na wengine huko chini mjini, na—na mahali mbalimbali, na kurudi kwenye moteli na hoteli, jalia tuseme kama wale waliotoka Emau kwenye ile asubuhi ya ufufuo, wakati ulipotembea pamoja nao siku nzima wala hawakukujua, uliwaelezea Neno la Mungu, na hata hivyo hawakukujua Wewe (Mara nyingi, hawa wakulima wa thamani na wapendwa ndio kwanza waone mauti mlangoni, na labda hawakutambua kwamba ni Wewe ndiye uliyefanya jambo hilo, ukayaokoa maisha yao.), lakini walisema, wale waliotoka Emau, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani?” Jalia tuseme vivyo hivyo. Jalia Yesu mtukufu, aliyefufuka aje mionganoni mwetu alasiri ya leo na kutuonyesha ya kwamba Yeye angali hai, na anatupenda, na hukutana popote wawili au watatu wamekusanyika pamoja. Tunaomba hayo, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

<sup>59</sup> Sasa, ningependa kusoma Andiko linalopatikana katika Kitabu cha Yohana Mtakatifu 12:20:

*Palikuwa na Wayunani kadha wa kadha mionganoni mwa watu waliokwea kwenda kuabudu kwenye sikukuu:*

*Basi hao walimwendea Filipo, mtu wa Bethsaida ya Galilaya, wakamwomba, wakisema, Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.*

<sup>60</sup> Halafu ninataka kuchukua somo langu kutoka Waebrania 13:8, *Yesu Kristo Yeye Yule Jana, Leo, Na Hata Milele*. Sasa, kumbukeni, ninanukuu Neno Takatifu la Mungu.

<sup>61</sup> Nami ninaamini ya kwamba hao Wayunani, siku hiyo, walifananisha swali lao na shauku yetu leo hii. Walikuwa wamesikia habari za Yesu, wala hakuna mtu anayeweza kusikia habari Zake, pasipo kupenda kumwona. Kama ningeweza kusema alasiri ya leo, “Ni wangapi katika jengo hili wangependa kumwona Yesu?” Nadhani kila mkono ungeinuliwa. Hebu tuone, ni wangapi wangetaka kumwona Yesu? Vema, hilo ni zuri sana. Asanteni.

<sup>62</sup> Ninaamini ya kwamba kila mtu anayepata kusikia habari Zake, hutamani kumwona, kwa sababu Yeye ni tofauti na mtu mwingine yeyote. Kamwe hapajakuwapo na mtu kama Yeye, na kamwe hatakuwapo. Kulikuwa na kitu tofauti na wanaafalsafa, wa wasomi wa Kiyunani wa siku hizo. Kulikuwa na kitu tofauti na kanisa na mapokeo ya Wayahudi.

<sup>63</sup> Yesu, kadiri tujuavyo, hakuwa na elimu ya duniani. Mtume Petro, hakuna hata mmoja wa wanatheolo-... wakuu wa Biblia, au, wanafunzi, aliyekuwa na elimu, isipokuwa Mtume Paulo. Naye alitwambia kwamba ilimbidi kusahau yote aliyowahi kujua kusudi amjue Yesu. Halafu basi akasema, tena, “Sikuja kwenu kwa maneno ya kushawishi ya wanadamu, ili imani yenu ijengwe katika,” kwa maneno mengine, “dhana za kiakili za wanadamu, bali nilikuja kwenu katika nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu, ili imani yenu iwe katika Mungu.”

<sup>64</sup> Tunaona Mtume Petro hakuwa na elimu ya kutosha kuandika jina lake mwenyewe, hata hivyo Yesu alimpa funguo za Ufalme. Yakobo na, ama, Petro na Yohana, wakipitia kwenye lango liitwalo Zuri, “Waliona kuwa walikuwa ni watu wasio na elimu wala maarifa, lakini waliwaangalia, wakijua ya kwamba walikuwa pamoja na Yesu.”

<sup>65</sup> Kwa hiyo hicho ndicho kitu tunachotazamia siku hizi, ni kuwa pamoja na kushirikiana na Yesu. Na kama ukiwahi kushirikiana Naye, kamwe hutakuwa vile vile tena. Hiyo ni kweli. Huwezi kuwa mtu yule yule kamwe ukiisha kushirikiana na Yesu wakati mmoja.

<sup>66</sup> Sasa, tunazungumza juu ya Utu huu mkuu wa Kristo, ambaye alikuwa ni Mungu katika mwili. Tu—tunanena habari Zake kuwa ni Mtu mkuu sana hata hakuna mtu duniani aliywahi kuwa kama Yeye wala kamwe asingeweza kuwako. Lakini basi tunashangaa ni kitu gani kilichompata Mtu huyu. Yuko wapi? Alipatwa na nini?

<sup>67</sup> Sasa, mara nyingi tunajaribu, kupitia...kwa...kwa kutokuamini, kueleza ya kwamba siku Zake zimekwisha, lakini hilo halitaridhisha Maandiko yaliyosema ni yeze yule jana, leo, na hata milele. Halafu basi, kama shauku yako leo, ni shauku

ile ile ambayo Wayunani hawa walikuwa nayo, "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu," nao wakapewa majaliwa hayo, walipata kumwona, basi, ikiwa *sisi* tunatamani kumwona Yesu, na kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, basi kwa nini *sisi* hatuwezi kupewa shauku hiyo?

<sup>68</sup> Ninaamini tunaweza, kwa sababu Yeye aliahidi, "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena." Sasa, *ulimwengu* hapo, kama vile hao ndugu, wasomi, wajuavyo, ya kwamba—ya kwamba *ulimwengu* hapo, linatokana na neno la Kiyunani *kosmos* ambalo linamaanisha "utaratibu wa *ulimwengu*." "Ulimwengu hautaniona tena, bali, ninyi," Kanisa, "mtaniona, kwa kuwa Mimi," *Mimi* ni kiwakilishi nafsi, "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Mnaona? Kote kote Yeye—Yeye, basi, hilo linamfanya Yeye yule yule jana, leo, na hata milele.

<sup>69</sup> Basi hana budi kuwa si yule anayefanana tu Naye, yule ambaye angekuwa kitu kama Yeye, bali hana budi kuwa yeze yule, yeze yule katika mtazamo, yeze yule katika nguvu, yeze yule katika kila kitu ila mwi—mwili wa kawaida; *ambao* umewekwa kwenye mkono wa kuume wa Mungu. Roho Wake yuko hapa, ndani yetu, kujidhihirisha Mwenyewe, na kuyachukua maisha yetu wenye kuya fanya jinsi hasa Yake yalivyokuwa. Hivyo ndivyo alivyoahidi, "Roho Mtakatifu, atakapokuja, atanishuhudia Mimi, na kuwaonyesha mambo yajayo." Mnaona? Sasa, tunajua hiyo ni kweli.

Basi, kama ningewaambia ninyi ndugu wa Kimethodisti, alasiri ya leo, "Mnaamini ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele?"

Mngesema, "Hakika kabisa, Ndugu Branham, kwamba, Yeye ni yule yule."

<sup>70</sup> Ningewaambia ninyi ndugu wa Kibaptisti, ama ninyi Wapentekoste, ama Wapresbiteri, ama Waanglikana, ama, loo, Wanazarayo, ama Wapilgrim Holiness, ama dhehebu lolote tunaloshiriki, "Mnaamini hilo?"

"Hakika, bila shaka ndivyo alivyo. Tunaamini ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele."

<sup>71</sup> Basi, je, Yeye ndiye Mponyaji? Yeye anafanya nini leo? Je, mnamwona kanisani mwenu kama tu alivyokuwa katika siku zilizopita? Sasa, hilo hapo swalii. Mnaona? Mnali kubali kutoka kwenye msimamo wa kiakili, dhana, lakini je, Yeye katika uhalisi ni yeze yule? Hilo ndilo jambo muhimu.

<sup>72</sup> Sasa, Biblia ilisema Yeye ni yule yule. Unasema, "Kufikia kiwango fulani ndivyo alivyo." Sasa, halisemi kwa eneo fulani, ilisema Yeye ni yule yule, yeze yule jana, leo, na hata milele. Ninajua hilo linasikika la kigeni sana, labda, kwa baadhi yenu, bali ninanukuu tu Maandiko. Ni, mimi siwajibiki kwa—kwa kuliandika, kamwe sikuliandika, bali Roho Mtakatifu

aliliandika, Naye anawajibika Kwalo. Jambo pekee nijualo, linasema Hivyo, nami sina budi kuamini Hilo kama mimi ni Mkristo, Sina budi kuamini kila Neno la Mungu ni Kweli, hakupaswi kuwepo na lolote lililoachwa nje hata kidogo.

<sup>73</sup> Sasa, huenda nisiwe na imani ya kutosha kuyafanya maneno haya yote yaishi tena, lakinia kamwe nisingemzuia mtu ambaye alikuwa na imani ya kufanya hivyo. Kama siwezi kutembea kama Henoko wala nisife, nifanye tu matembezi ya alasiri na kwenda Nyumbani kwa Mungu bila ya kufa, kama sina imani kama hiyo kamwe nisingeweza...ningemshukuru Mungu kwa ajili ya mtu ambaye alikuwa na imani kiasi hicho kufanya jambo hilo. Kamwe ningesema lisingeweza kutendeka, kwa sababu ni Neno la Mungu.

<sup>74</sup> Sasa, kama Yeye ni yule yule, basi, nasi tunatamani kumwona, basi hatuna budi kumwona Yesu yeye yule waliywona, kama Yeye anadumu yeye yule. Sasa, hilo linasikika la kiakili, sivyo? Sasa, hebu tuone ni nini...

Sasa, kama ningesema, “Ninyi ndugu wa Kimethodisti mnaamini hilo? Mbaptisti? Na kama nilivyolinukuu?”

“Naam.” Vema, sasa, njia pekee...Mnasema, “Yuko kanisani mwetu.”

“Yuko kanisani mwetu.”

<sup>75</sup> Vema, nasema, “Hiyo ni kweli. Ninaamini hilo.” Lakini hebu tuone, njia pekee ya kuwa sahihi juu yake, kulihusu, kulifanya Neno kweli au la, ambalo, ni kweli, ni kurudi nyuma na kuona kile alichokuwa. Na kama tunaweza kujua kile alichokuwa, basi tutaona kile alichokuwa, halafu kile atakachokuwa daima. Hiyo ni kweli? Hilo linasikika wazi nya kutosha? Mnaona? Kile alichokuwa, ndicho alichokuwa.

<sup>76</sup> Vema, sasa, kama tungeweza kuingia leo hii kumtafuta Yesu, tungemwendea mtu wa aina gani? Naye angekuwa ni Roho wa aina gani, kama tungeingia makanisani mwetu kumtafuta? Hebu twende tukichunguza kila moja la hayo, tuone kile tunachoweza kupata.

<sup>77</sup> Je, tungemwona mtu mwenye ukosi uliopinduliwa, na kilemba kichwani mwake, ama—ama kitu kama watu wetu mashuhuri, *wanaojiita*, watu watakatifu walivyo siku hizi? Si Yesu, Yeye alivalia tu kama watu wa kawaida, aliingia na kutoka mionganoni mwa watu, amevalia tu kama wanadamu walivyovalia.

<sup>78</sup> Tusingemtafuta mwanachuoni fulani mwenye akili. Hatuna rekodi yoyote kwamba aliwahi kuhudhuria shule siku moja. Vema, tungeangalia nini basi? Tungemtazamia Masihi, Mtiwa Mafuta.

<sup>79</sup> Sasa, kwenye, sasa, nimesoma kutoka Yohana Mtakatifu 12. Sasa, tunapoendelea tutayachunguza Maandiko, siku, ama, mkutano baada ya mkutano, kuonyesha mambo haya

vizuri. Sasa, tulianzia katika Yohana Mtakatifu, hebu turudi tu mwanzoni mwa Yohana Mtakatifu. Usipoyasoma papa hapa, unaweza kuyasoma nyumbani, ukiandika manukuu. Basi hebu turudi nyuma sasa tuone Yesu alikuwa ni nani. Na kama tunaweza kujua kile alichokuwa, Naye atajithibitisha Mwenyewe kuwa yeze yule leo, je, ingewafurahisha? Nyote mtafurahia sana jambo hilo, kama lingemfanya Yeye yule leo?

<sup>80</sup> Sasa, tumeninii, nimesimama katika nchi za kigeni nikiwa na Kurani katika mkono mmoja, ya dini ya Kiislamu, ambayo ni moja ya zilizo kuu sana ulimwenguni, na pamoja na kitabu cha Buddha, na Biblia katika kila mmoja, katika mkono *huu*, na kusema, “Mtu fulani hana budi kuwa amekosea, kuna tofauti nyingi sana, mtu fulani hana budi kuwa wa kweli, kama kuna Mungu. Sasa, hebu na tuthibitishe tuone ni kipi kilicho sahihi.” Mnaona?

<sup>81</sup> Kamwe usiogope kumleta kwenye Neno la Mungu kwenye shindano la kuamua. Daima atakuwepo. Na kwa hiyo, iweni tu na imani na kumwamini. Usijaribu kuongeza kitu au kuondoa Kitu Kwake, liamini tu jinsi nilivyoandikwa na useme, “Liko hivyo.” Ndipo uamini Hilo pasipo kivuli cha shaka, ndipo Mungu anawajibika, kama kweli unaliamini, si kujifanya kuamini. Sasa, yeze hatadanganya, Shetani si mdanganyifu, yeze ni mdanganyifu, bali kama anaweza kukudanganya atafanya hivyo, lakini unapokuja na imani halisi, yeze anajua kama unadanganya au la. Unaona?

<sup>82</sup> Wakati wanafunzi walipopewa nguvu za kuwaponya wagonjwa, siku kumi baadaye tunawaona wakishindwa na ugonjwa wa kifafa. Nami ningewazia Petro akisema, “Ngojeni, nitawaonyesha jinsi nilivyoofanya huko Kapernaumu.”

Na huyo mwingine akisema, “Nitawaonyesha jinsi nilivyoifanya.”

<sup>83</sup> Wala hakuna hata mmoja wao angaliweza kumfanya huyu pepo amwache huyo mtoto. Lakini wakati Yesu alipokuja, naye baba yake akaenda kumwona Yesu, naye akasema, “Nimemleta kwa wanafunzi Wako nao hawakuweza kumfanya chochote, ndipo nikamleta Kwako.”

<sup>84</sup> Akasema, “Ninaweza, kama ukiamini, kwa kuwa mambo yote yanawezekana kwao waaminio.” Ndipo huyo mtoto akashikwa na kifafa kibaya sana alichopata kuwa nacho, maana ibilisi huyo alijua ya kwamba alikuwa amekutana na imani katika kiwango tofauti na kile walichokuwa nacho mitume; alikuwa amekutana na imani kamilifu.

<sup>85</sup> Hiyo ndiyo tunapaswa kuwa nayo: imani kamilifu kulifanya Neno kamilifu la Mungu litekeleze kikamilifu. Jambo ndilo hilo. Hatuna budi kuliamini bila shaka lolote.

<sup>86</sup> Sasa, hebu na turudi huko chini Galilaya, tuchukue safari ndogo ya akili sasa kwa yapata dakika ishirini. Hebu twende

Galilaya tuone Yesu alikuwa ni nani. Tunajua kuzaliwa Kwake na kuchukuliwa Kwake mimba pasipo na dhambi na jinsi Yeye alivyozaliwa.

<sup>87</sup> Naye Yohana akaenda nyikani, ule umri, yapata umri wa miaka tisa, huku akiomba na kufunga mbele za Mungu, na umri wa miaka thelathini, alitoka akihubiri, "Masihi ajaye." Ndipo siku moja, maskini Mtu wa kawaida akashuka ukingoni, bali kulikuwako na ishara juu Yake ambayo ilikuwa ni ishara ya Masihi, ndipo Yohana akaitambua. Naye akasema, "Nilijua ya kwamba alikuwa Ndiye, kwa kuwa nilionia ishara ambayo, iliniambia huko nyikani, kwamba, Yeye angekuwa ni nani.

<sup>88</sup> Yesu, alibatizwa na Yohana, ndipo tunaona ya kwamba siku arobaini alijaribiwa na ibilisi nyikani. Ndipo baada ya Yeye kutoka katika majaribu yake, tunamwona mara moja akiingia katika huduma Yake ya umma. Sasa, hivyo ndivyo tulivyo, hapa alasiri ya leo, tukiingia katika huduma Yake ya umma. Nao wagonjwa wakaanza kuponywa wakati alipowaombea. Ndipo ikasababisha vurugu kubwa mionganoni mwa makanisa. "Mtū huyu ni nani?" Hawakuwa na jibu katika—katika kanuni zao za imani. Nao—nao walikuwa, wasingeweza kukana kwamba ja—jambo muhimu lilikuwa likifanyika.

<sup>89</sup> Kwa hiyo kulikuwa na maskini mvuvi jina lake Andrea, naye alikuwa na ndugu mmoja jina lake Simoni. Naye Andrea akajaribu kumfanya Simoni auhudhurie ule mkutano, na hatimaye Simoni akakubali, siku moja, kwenda. Ndipo wakati Simoni alipokuja Mbele za Bwana Yesu, sasa angalieni kwa makini, alipomjia Bwana Yesu, hakumwuliza kama alikuwa na, Shahada Yake ya Sanaa bado, ama hakumwuliza Yeye alikuwa wa dhehebu gani, alitembea tu, kama ulivyofanya, kama nilivyofanya mimi, na mara macho ya Yesu yalipomtazama, Yeye alisema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona."

<sup>90</sup> Simoni akashangaa sana, kwa sababu baba yake Yona alikuwa Mfarisayo, mtu mashuhuri. Na kama umesoma historia, alijaambia wanawe ya kwamba siku moja Masihi atakuja, halafu wote walikuwa wakimtzamia Masihi. Mnajua walidhani Yohana alikuwa Masihi? Kwa sababu kanisa halisi la kweli lilikuwa likimtzamia Masihi. Basi kumbukeni, Yeye huja tu kwa wale wanaomtzamia, Yeye huwaokoa tu wale wanaoamini ya kwamba anawenza kuwaokoa, Yeye huwaponya tu wale wanaoamini ya kwamba anawaponya.

<sup>91</sup> Naye Simoni, akimtzamia Masihi, alikuwa ameahidiwa kwa miaka elfu nne, tangu Edeni. Manabii walikuwa wamenena habari zao. Waliishi kwa torati ya Musa. Naye Musa, na, ungetaka kulirejea, Kumbukumbu la Torati 18:15-22, maneno yake katika nukuu kwa Israeli, alisema, "Bwana Mungu wenu, atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi; itakuwa kwamba

yejote asiyemsikia Nabii huyu atakatiliwa mionganoni mwa watu."

<sup>92</sup> Sasa, Israeli wote, waliofundishwa katika Neno, sasa msisahau hili, enyi darasa, walijua ya kwamba Masihi alikuwa awe nabii. Sasa, Israeli walipaswa kuwasikia manabii wao. Biblia ilisema, Mungu akinena na Israeli, "Akiwepo mtu mionganoni mwenu aliye wa rohoni au nabii, Mimi Bwana Mungu nitajifunua Mwenyewe kwake katika ono, nitasema naye katika ndoto. Na kama yale nabii huyu asemayo yakitimia, basi msikieni nabii huyo, lakini lisipotimia, msimwogope nabii huyo, kwa sababu mimi siko pamoja naye, lakini kama yale asemayo yakitimia, basi iweni waangalifu, nimemtuma nabii huyo."

<sup>93</sup> Yohana, basi, walijua ya kwamba yeje alikuwa ni nabii, kwa sababu alikuwa amewaambia yatakayokuja, na kumtambulisha Ma—Masihi. Sasa, Masihi huyu alikuwa awe na ishara, na ishara hiyo ilikuwa ni Mungu-Nabii. Yeye hakuwa tu nabii, bali alikuwa Mungu-Nabii. Alikuwa ndiye Mungu wa manabii, lakini ishara yake ya Masihi ilikuwa ni kufanya ishara ya nabii.

Unajua walisema, "Hebu tukuone ukifanya ishara ya nabii, tutakuamini," mnaona, walipoweka kitambaa juu ya uso wake.

<sup>94</sup> Lakini alikuwa hapa kwa Wateule, kwa mtu ambaye angeamini, Simoni, hakuwa amewahi kuona maishani mwake, ama kumwona, naye akamkazia macho na kusema, "Tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye ndani yake mna . . ." la, samahani, Akasema, "Jina lako ni Simoni, mwana wa Yona. Tangu sasa utaitwa Petro."

<sup>95</sup> Ninawazia hilo lilimwondolea majivuno huyo Farisayo, wakati alipomwona Mtu huyo ambaye kamwe hakumwangalia, ama hakuwahi kumwona maishani Mwake, akimwambia yeje alikuwa ni nani, jina lake ilikuwa nani, kwamba baba yake alikuwa ni nani. Sasa, hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi. Huyo alikuwa ni Yesu jana. Hivyo ndivyo alivyojitambulisha kwa watu kama Masihi.

<sup>96</sup> Sasa, kulikuwako na mmoja aliyesimama pale jina lake Filipo, ningali katika mlango wa kwanza wa Yohana Mtakatifu, mtu jina lake Filipo, mtu mwema, mtu mwenye haki, aliona jambo hili likitukia. Na kuna jambo fulani kulihusu, unapomwona Yesu akija jukwaani, kamwe huwezi kutulia, huna budi kumwambia kila mtu habari zake, hiyo ni kusema, kama unampenda. Kwa hiyo Filipo, loo, alifurahi *sana* hata akasema, "Sina budi kwenda kumwambia Nathanaeli, rafiki yangu."

<sup>97</sup> Sasa, wengi wenu ndugu hapa, huenda mmekuwa Palestina. Kama mtaangalia mahali ambapo Yesu alikuwa wakati huo, mpaka ambapo Nathanaeli alikuwa, ni kama maili kumi na tano kuuzunguka mlima. Ndipo Filipo akaenda mbio akauzunguka huo mlima akampata Nathanaeli. Na hebu *tuliigize* hapa, kwa dakika moja tu, mchezo mdogo wa kuigiza.

<sup>98</sup> Ninaweza kumwazia akienda hadi mlangoni, na kubisha mlangoni. Ndipo Bibi Nathanaeli akaja mlangoni naye akasema, “Yuko wapi Nathanaeli?”

“Loo, anatembea katika shamba lake la matunda.”

<sup>99</sup> “Lazima nimwone mara moja.” Huyo akarudi bustanini. Hapo anamwona Nathanaeli amepiga magoti, chini ya miti, akiomba, labda, “Ee Mungu,” kitu kama hiki, labda, “tumetamani na kumngoeja huyo Masihi ajaye. Tunaamini ya kwamba Wewe utamtuma siku moja. Tu—tunaamini hilo, Bwana, nami nitakuwa nikimtzamia atakapokuja. Amina.”

<sup>100</sup> Sasa, Filipo, akiwa mwungwana Mkristo, asingeyakatiza hayo maombi, la hasha, alisimama kwa uchaji mpaka Nathanaeli alipomaliza kuomba. Ndipo anainuka, Nathanaeli, na kuanza kupangusa vazi lake. Na upesi, kamwe hakusema, “Mazao yanaendeleaje?” ama . . . Huo u—u—ujumbe ulikuwa wa dharura, hana budi kuufikisha kwake upesi sana.

<sup>101</sup> Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, ndugu. Ujumbe, hatuna muda wa miaka kumi na mitano ya masomo, huu Ujumbe ni wa dharura, ulimwengu uko mwisho, wakati umewadnia. Mambo yaya haya mtakayoonaa katika mkutano huu yanathibitisha ya kwamba hatua inayofuata ni kule kuja kwa Bwana, kule kuhamishwa kwa Kanisa, Kimaandiko.

<sup>102</sup> Sisemi jambo hilo ili kusababisha hofu, ninasema hilo kama onyo ili muwe tayari. Hatujui ni dakika gani anayoweza kuja.

<sup>103</sup> Sasa, angalieni kilichotukia. Alisema, “Njoo, umwone Yule tuliyempata, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu.”

<sup>104</sup> Naye Filipo akamwambia Nathanaeli maneno haya, naye Nathanaeli alikuwa mwothodoksi hodari, mwajua, kwa hiyo, mgumu sana, nadhani, akasema, “Sasa,” kitu kama hiki, “ngoja kidogo, laweza neno lolote jema kutoka Nazareti?” Na, labda, kwamba huenda alisema hivi: “Sasa, kama kungekuwa na kitu kama hicho kinachokuja, vema, bila shaka kingekuja kupidia kwetu sisi Mafarisayo, ama Masadukayo walisema, ‘Kingekuja kupidia kanisani mwetu.’ Na kama kilikuwa kinakuja, vema, bila shaka, ushoroba wa Mbingu ungefunkuwa, na—naye Masihi angeshuka moja kwa moja juu ya, karibu na hekalu, Naye angesema, ‘Kayafa, mheshimiwa kuhani mkuu, mimi huyu hapa.’”

<sup>105</sup> Lakini mnaona, Mungu hafanyi mambo namna hiyo, kamwe hakufanya hivyo, wala kamwe hatafanya, Yeye huja na kuchukua vitu bubu vyta ulimwengu na kufanya kitu kutoka kwake, na kujithibitisha Mwenyewe, kutimiza Neno Lake. Sasa, yachunguzeni Maandiko mwone kama hiyo si kweli. Yeye huchukua kitu kisicho na maana.

<sup>106</sup> Alipowaita mitume Wake, alichukua nini? Wavuvi, watu wasio na elimu. Kwa nini Yeye hakuwachukua waliostaarabika?

Kwa nini hakuwachukua makuhani? Walikuwa na wahudumu wa siku hiyo ambao wangezidi kwa mbali chochote ambacho tumewahi kuwa nacho. Ilibidi wawe, watoke kwenye ukoo wa Walawi wapate kuwa makuhani, baba wa babu wa babu wa babu wa babu wa babu zao walikuwa makuhani. Basi kwa nini Yeye hakuenda kwa wa aina hiyo? Lakini mnaona, Yeye alichukua kitu fulani, kitu duni, kuthibitisha ya kwamba Yeye ni Mungu, ya kwamba anaweza kufanya kitu fulani kutoka kwa kisichokuwapo.

<sup>107</sup> Na upesi, ama, mara mimi na wewe tunapoweza kutambua ya kwamba sisi si kitu, hivyo ndivyo Mungu anavyoweza kutenda kazi pamoja nasi upesi, tunapoondoaa dhana zetu za kiakili kutoka kwake, na kusema tu, “Mungu, naamini, saidia kutokuamini kwangu.” Jambo ndilo hilo. Kama Neno linasema hivyo, basi ni kweli. Mungu yuko nyuma ya Neno Lake, Naye yuko katika Neno Lake, Naye ni Neno.

<sup>108</sup> Sasa, tunaona ya kwamba huyu mwothodoksi hodari alimwangalia na kusema, labda kitu kama hiki, “Sasa, Filipo, nimekujuu kuwa mtu mzuri. Tumeenda kanisani pamoja kwa miaka mingi, lakini naamini umerukwa na akili. Lazima una kasoro, umekuwa na namna fulani ya fikra za uwongo. Unataka kuniambia ya kwamba mtu kutoka Galilaya angekuwa ndiye Masihi? Je, huyo ndiye yule Mtu, niliyesikia, aliyezaliwa mwana haramu, yule Mtoto mchanga, miaka mingi iliyopita, waliyenena habari zake? Kwanza kabisa yuna jina jeusi, na hapa unakuja ukiniambia ya kwamba Huyu amegeuka kuwa ndiye Masihi. Loo, Filipo, jirudie. Laweza neno lolote jema kutoka Nazareti?”

<sup>109</sup> Nafikiri alimpa jibu ambalo lingetukomesha sisi sote, alimpa jibu sahihi, akasema, “Njoo uone.” Jambo ndilo hilo. Usikae nyumbani na kukosoa. Lete Biblia yako uone kama ni kweli. Hilo ni fundisho zuri kwetu. “Njoo, uone.”

<sup>110</sup> “Yachunguzeni Maandiko,” Yesu alisema, “kwa kuwa Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi.”

Sasa, “Njoo, uone.”

<sup>111</sup> Ninaweza kuwazia, walipokuwa wakianza kurudi, wafike kesho yake, ni maili kumi na tano, labda iliwachukua safari ya siku mbili kurudi, ninaweza kuwazia barabarani, hebu na tuyalingilie mazungumzo yao, hatutakuwa wasio wa kimaandiko sasa, kwa hiyo basi, katika mazungumzo yao, ninaweza kumsikia Filipo akisema, “Basi, Nathanaeli, usingeweza kuamini hilo? Bwana, ndugu yangu, wewe ni mwanatheolojia, wewe ni mtu mwenye mamlaka katika Maandiko, unasoma nini juu ya Masihi? Masihi atakuwa nini wakati atakapokuja? Tutamtafuta Mtu wa aina gani?”

“Loo,” alisema Nathanaeli, “Yeye atakuwa ni Nabii, kwa sababu Biblia ilisema Yeye atakuwa ni Nabii, Maandiko yetu matakatifu yanasema Yeye atakuwa Nabii.”

<sup>112</sup> “Vema, unamkumbuka yule mvuvi mzee ambaye ulinunua samaki kwake siku ile, jina lake Simoni, naye hakuwa na elimu ya kutosha kuandika jina lake mwenyewe?”

“Naam, ninakumbuka hilo vizuri.”

<sup>113</sup> “Alikuja mbele ya huyu Yesu wa Nazareti, naye Yesu wa Nazareti akamwambia ye ye ni nani, na si hilo tu, bali alimwambia maskini yule baba yake mtauwa alikuwa ni nani. Wala halingenishangaza, lakini, kama Yeye hakukwambia wewe ni nani.”

<sup>114</sup> Vema, ninaweza kumwazia Nathanaeli akisema, “Kama ndivyo ilivyo, sijui, sijawahi kuwa kule, lakini kama hiyo ni kweli, Huyo atakuwa ni Masihi, kwa sababu hivyo ndivyo anavyopaswa kufanya, Yeye ni Nabii. Wala hatujawa na nabii,” akasema, “kwa miaka mia nne, tangu tulipokuwa na nabii, nasi tumekuwa tukimtzamia Masihi huyu, ambaye ndiye anayefuata.”

Hatujawa na mmoja kwa miaka elfu mbili. “Sasa . . .” Lakini tunamtazamia mmoja.

“Sasa,” akasema, “Masihi huyu, kama Yeye ni Masihi, basi nitamwona akifanya ishara.”

<sup>115</sup> Ndipo tukaingia kwenye kusanyiko, nadhani, na labda alikuwa kwenye mstari wa maombi, ama labda alikuwa amesimama kwenye kusanyiko, sijui. Lakini, hata hivyo, mara Yesu alipogeuka na kumwangalia, Yeye alisema, “Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!”

<sup>116</sup> Sasa, kwa mfano mkosoaji anaweza kuwapo, wangesema, “Vema, hakika, alikuwa amevaa kama yeye.” Loo, la, watu wa mashariki wote wanavalia sawa, wana joho refu, na vazi la ndani, na kilemba, na wana ndevu, kwa hiyo alikuwa, asingeweza kumwambia, angaliweza kuwa ni Myunani ama chochote kile.

Akasema, “Tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake!”

<sup>117</sup> Ninaweza kuwazia ule ugumu ukimtoka upesi sana. Naye akasema, “Rabi,” ambalo linamaanisha *mwalimu*, “ulipata kunijua lini Wewe? Hii ndiyo mara ya kwanza ambayo tumewahi kukutana, basi Wewe ulijuaje kwamba nilikuwa Mwisraeli, mtu asiyie na hila?”

<sup>118</sup> Sikilizeni! Akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Ni macho ya jinsi gani!

Mwaminio huyu mwaminifu, aliyejua Maandiko, alisema nini? “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.”

Yesu akasema, “Kwa sababu nilikwambia hivyo, unaamini? Utaona mambo makubwa zaidi, sasa.” Unaona?

<sup>119</sup> Sasa, huyo alikuwa ni Yesu jana, jinsi alivyo jitambulisha Mwenyewe kwa watu kama Masihi. Kama Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele, hivyo ndivyo angekuwa leo, kama Yeye ni yeye yule. Je, hiyo ni kweli? Lazima iwe.

<sup>120</sup> Sasa, kuna manukuu mengine mengi tungeweza kuyanukuu, lakini ninii... Ninajua hatuna ila kama dakika arobaini na tano zaidi. Nami nitalishika kupidia kwenye Maandiko.

<sup>121</sup> Lakini ninapenda kwenda kwenye, hebu tuseme hivi, kuna jamii tatu za watu duniani. Ninajua mnasema, "Mimi ni wa *hii, ile*, ama *nyingineyo*." Lakini kuna jamii tatu tu, sote tulitokana na wana wa Nuhu, Maandiko ni kweli: Hamu, Shemu, na Yafethi. Sasa, hizo ziligeuka kuwa katika siku Zake, Myahudi, Mmataifa, na Msamaria.

<sup>122</sup> Sasa, tunaona ya kwamba kulikuwako na jamii ya watu walioitwa Wasamaria, ambao ni nusu Myahudi na Mmataifa. Nao walikuwa wakimtzamia Masihi. Walitaka kumwona Masihi.

<sup>123</sup> Sasa, kumbukeni, kulikuwa na wale waliosimama pale waliomwona Yesu akifanya hivyo. Mnajua walichosema? Walikuwa wahubiri mashuhuri, waalimu mashuhuri, waothodoksi katika imani yao, lakini walisema, "Mtu huyu ni Beelzebuli. Yeye ni mpiga ramli." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

<sup>124</sup> Yesu aliwaambia nini? Hawakusema kwa sauti, bali Yeye aliyatambua mawazo yao. Sote tunajua hayo ni Maandiko. Alitambua mawazo yao, kisha akawageukia, naye akasema, "Nitawasamehe hilo," hayo mawazo mabaya, kuziita kazi za Mungu pepo mchafu, Beelzebuli, mpiga ramli. Siku hizi, wangeziita kitu kama hicho, ama telepathia, bali jina bayaa kwa kazi za Mungu. Yeye alisema, "Lakini siku moja Roho Mtakatifu atakuja kufanya jambo lile lile," sasa, hapa ndipo linapotuweka, "neno moja dhidi Yake, halitasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao." Hivyo ndivyo lilivyo takatifu. "Neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao."

<sup>125</sup> Kwa hiyo mnaona, kama Yeye anafanya jambo hili, linatuweka mahali gani. Linatutia muhuri upande mmoja au mwininge. Wakati wa kutenganisha umewadnia, ile hukumu ya kupeleleza.

<sup>126</sup> Sasa, tunaona mahali pengine engi, tutachukua mlango ufuataao, vema, sisi, kwanza, hebu twende, sasa, kuna Myahudi, Mmataifa, na Msamaria. Sasa, hata wakati mmoja hakufanya ishara hiyo mbele ya Mmataifa. Huwezi kulipata katika Maandiko. Mataifa tulikuwa, sisi Waanglo-Sakson, Wamataifa, hatukuwa tukimtzamia Masihi ye yeyote kuja. Tulikuwa na marungu mgongoni mwetu na kuabudu sanamu, mnaona, makafiri, Warumi, na kadhalika.

<sup>127</sup> Sasa, lakini Yeye huwajia wale wanaomtazamia. Alifanya hivyo katika siku hiyo. Kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, atafanya hivyo tena leo. Anawajia wale wanaomtazamia, wale wanaotamani, kama wale Wayunani walivyokuwa, “Sisi tunataka kumwona Yesu.”

<sup>128</sup> Sasa, Yeye alikuwa akienda zake Yeriko, ambao ulikuwa chini ya mlima, ambapo Yerusalemu iko juu ya mlima, bali Yeye alisema alihitaji kuitia Samaria, sasa, ya mji wa Sikari. Sasa, tunaona ya kwamba Samaria iko barabaran *hivi*, unapanda upande *huu* kisha unashuka kwenda Yeriko, mbali sana na njia Yake. Lakini alienda kwenye mji *huu* fulani wa Samaria, wa Samaria, naye akaketi chini na kuwatuma wanafunzi Wake waende wakanunue chakula.

<sup>129</sup> Basi walipokuwa wameondoka, kulikuwa na mwanamke mwenye, vema, mwenye sifa mbaya, tungemwita Marekani, hapa, kwamba alikuwa ni mwa—mwanamke mwenye sifa mbaya. Ni wangapi wanaojua alikuwa na shida gani? Alikuwa amevunja nadhiri yake ya ndoa, alikuwa na waume watano. Na labda, hebu tuseme, alikuwa ni mwanamke mrembo. Na kila mtu alikuwa ameondoka. Na kama uliwahi kuwa kule, kile kisima bado kingalipo, ni mandhari ndogo, kitu kama *hiki*.

<sup>130</sup> Naye Yesu, Yeye alikuwa na umri wa miaka thelathini tu, ama, haikufika thelathini na mitatu kabisa, lakini hata hivyo, hapana shaka alionekana mwenye umri mkubwa zaidi. Wakati alipokuwa akizungumza, katika Yohana Mtakatifu 6, na Wayahudi walipokuwa na karamu, nao walikuwa wakinywa maji haya, yakiwakilisha yale maji kutoka kwenye ule mwamba uliopigwa nyikani, Yeye akasema, “Mimi ndimi ule Mwamba uliokuwa nyikani.”

<sup>131</sup> Loo, wao, loo, hilo lilichochea hasira yao ya haki, nao wakasema, “Unataka kuniambia ya kwamba ulimwona Ibrahimu, nawe ni mtu asiyezidi umri wa miaka hamsini?” Alionekana mwenye umri wa miaka hamsini, bali alikuwa na thelathini tu. Kazi Yake labda ilimfanyia Yeye, labda kidogo anaingia mvi ama chochote kile.

<sup>132</sup> Vema, Yeye alijaambia nini? “Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.” Yeye alikuwa ni Mungu wa Ibrahimu, lakini Huyo hapo, amevaa tu nguo kama mtu wa kawaida. Kwa hiyo Mtu huyo huenda alionekana kidogo amezeeka.

<sup>133</sup> Lakini Yeye alikuwa ni Myahudi, na kulikuwa na ubaguzi, kama vile tulivyo na mzozo huko chini Louisiana na Georgia, ninao marafiki fulani wa Georgia wanaoketi hapa, kuhusu ubaguzi... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] ...weusi na weupe, na kadhalika, hao walikuwa ni Wayahudi na Wasamaria.

<sup>134</sup> Na kwa hiyo Yesu alimwona yule mwanamke akija na, vema, labda kama uliwahi kuwa huko mashariki, desturi zao hazibadiliki, sawasawa, asingweza kutoka na wanawake

waadilifu. Mnaona, inawabidi kutoka, ninii, mapema, wanawali wanatoka mapema na kuteka maji yao.

<sup>135</sup> Nami nimewaona wakichukua mtungi wake, utaenea galoni tano, wakauweka kichwani mwao, na kuweka mmoja kwenye kila nyonga, na kuendelea namna hiyo, wakizungumza tu kama vile kina mama wanavyoweza kufanya, mwajua, na kamwe hawatamwaga hata tone la maji. Ni—ni ajabu kuona jinsi wanavyotembea kwa ukamilifu na unyofu na huo, wakiongea tu wao kwa wao, mwajua, pasipo kuusogeza mtungi huo mkubwa wa maji kichwani mwake. Vipini viwili vikubwa juu yake, ambapo wanaushusha, wanauingiza kisimani wakachote maji.

<sup>136</sup> Basi msichana huyu anakuja huko nje, yeze labda, amebeba kile chungu nyongani mwake, kama kawaida kwa kulabu chini ya mkono wake. Naye alikuwa akiwazia, labda, kuhusu yale aliokuwa amefanya usiku uliotangulia, asingeweza kushirikiana na wanawake wazuri. Kwa hiyo akaanza kushusha huo mtungi ki—kisimani. Naye akasikia...akasikia Sauti ikisema, “Nipe maji ninywe, ewe mwanamke, nipe maji ninywe.”

<sup>137</sup> Naye akageuka, naye Myahudi wa makamu ameketi karibu na mizabibu ameegemea ukutani. Upesi akasema, “Si kawaida kwa Myahudi kumwomba mwanamke Msamaria fadhili yoyote.” Loo, ubaguzi ulikuwa mkali. “Hatuna uhusiano sisi kwa sisi. Na Wewe ni Myahudi, na mimi ni mwanamke Msamaria, ungeweza je kuniomba maji ya kunywa?”

<sup>138</sup> Sikiliza jibu, “Mwanamke, kama ungejua ni Nani uliyekuwa unasesma naye,” loo, jamani, hivyo ndivyo ilivyo leo, “kama ungalijua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe. Ningekuletea maji, ama, kukupa maji, usije hapa kuteka.”

“Loo,” akasema, “kisima ni kirefu, wala huna chochote cha kuchotea.”

<sup>139</sup> Ndipo mazungumzo yakaendelea. Yesu alikuwa akifanya nini? Sasa, hapa, itawabidi kuamini neno langu, natumaini mtaliamini, Yeye alikuwa akiwasiliana na roho yake. Alijua kulikuwa na kasoro fulani. Baba alikuwa amemtuma huko juu, kwa hiyo alijua mwanamke huyu alikuwa anakuja, kwa sababu Yeye alisema, katika Yohana Mtakatifu 5:19, “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezu kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda.” Mnaona?

<sup>140</sup> Sasa, hapana shaka Baba alimtuma huko juu, Naye akaona huyo alikuwa ni yule mwanamke, kwa hiyo ilimbidi kuwasiliana na roho yake kuzungumza naye, ili apate kujua shida yake ilikuwa wapi, akasema...

<sup>141</sup> Akasema, “Sisi tunaabu—...Ninyi mnaabudia Yerusalem; na katika mlima huu, sisi tunaabudu...” Mazungumzo yakaendelea kwa muda mrefu kidogo, hatimaye, Yesu akapata

shida yake. Sasa, sikilizeni, samahani, sijaribu kuwapigia makelele, nimekuwa nikihubiri huko nje, na kadhalika, basi ninapiga kelele nyigi sana, nafikiri. Kasema, "Huna kitu cha kuchotea, kwa hiyo ungewezaje kupata maji?"

<sup>142</sup> Kasema, "Vema, sasa, kama ulijua ni Nani uliyekuwa unasesma naye, ungeniomba Mimi maji unywe, ningekupa maji usije hapa kuchota." Ndipo mazungumzo yakaendelea, Yeye akasema, "Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa."

Loo, ninaweza kuona macho yake yakichangamka. Akasema, "Sina mume." Ni m-mshtuko wa jinsi gani.

Akasema, "Umesema vema. Umekuwa na waume watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako, kwa hiyo umesema vema."

<sup>143</sup> Msikilize huyu kahaba, mwanamke mwenye sifa mbaya, alijua zaidi juu ya Mungu kuliko nusu ya wahubiri Marekani. Kamwe hakusema, "Wewe ni Beelzebuli, ibilisi." Alisema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii." Sasa, sikilizeni, "Tunajua, sisi Wasamaria, tunajua ya kwamba Kristo yuaja, aitwaye Masihi, yuaja, aitwaye Kristo, Mtwa Mafuta," mnaona, "na ajapo hii itakuwa ndiyo ishara atakayoonyesha, Yeye atatuambia mambo haya. Wewe ni Nabii, bali tunamtazamia Masihi, basi ajapo Masihi huyu, Yeye atatuambia mambo haya, hii itakuwa ndiyo ishara Yake."

<sup>144</sup> Loo, enyi kanisa, mnawenza kuliona? Huyo ndiye Masihi, hiyo ndiyo ishara ya Masihi. Mnaona? "Tunajua ya kwamba ajapo Yeye atatuonyesha mambo haya." Yeye kamwe...hakusema kamwe, "Wewe ni Beelzebuli, hapana shaka wewe ni mpiga ramli." Yeye...

<sup>145</sup> Sasa, hivyo ndivyo wahubiri walivyomwita, makasisi wakubwa katika siku hiyo, makuhani, walisema, "Jamaa huyo ni mwa—mwa—mwanatelepathia, yeye a—anatumia akili, kiakili, yeye—yeye ni mpiga ramli."

<sup>146</sup> Yesu akasema, "Ninawasamehe, lakini siku moja Roho Mtakatifu anakuja kufanya hivyo. Ukisema neno moja dhidi Yake, hutasamehewa kamwe."

<sup>147</sup> Na siku hiyo imewadia, sasa; akizungumza na kizazi kingine.

<sup>148</sup> Angalia, alisema, kwa unyenyekevu, "Bwana, hapana shaka Wewe ni nabii. Tunajua, sisi Wasamaria, tunamtazamia Masihi kuja, na Masihi huyu ajapo, Yeye atatuonyesha ishara ya kwamba Yeye ndiye Nabii mkuu sana." Mnaona? "Tu—tunajua ajapo tu—tutajua ya kwamba Yeye ni Nabii, kwa sababu atafanya ishara hizi."

<sup>149</sup> Hebu msikilizeni: "Mimi ninayesema nawe Ndiye." Kamwe hapajakuwapo na mtu hapo awali wala hakuna hata mmoja baada ya hapo angeweza kusema hivyo. "Mimi ninayesema nawe Ndiye."

<sup>150</sup> Kusikia hayo, akaangusha mtungi wake wa maji na kukimbia mjini na kusema, “Njoni, mwone Mtu,” sasa, sikilizeni, enyi darasa, ninyi wasomaji wa Biblia, “njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?”

<sup>151</sup> Nao wakatoka wakamsihi aingie mjini. Nayo Biblia ilisema ya kwamba watu wa mji huo, hao watu, walimwamini kwa sababu ya ushuhuda wa huyo mwanamke.

<sup>152</sup> Je, hiyo inaweza kuwa ni udanganyifu? La, bwana. Hayo ni Maandiko, sivyo. Vema, kama huyo alikuwa ni Yesu jana, ni Yesu leo.

<sup>153</sup> Sasa, angalieni, sote tunajua sasa, ya kwamba huko kulikuwa ndiko kumalizia kwa siku ya Wayahudi. Walimkataa Masihi wao, tunajua hilo. Sasa, walikuwa wakimtazamia Masihi, na wakati Masihi alipokuja, Yeye akakataliwa. Na wakati alipofanya ishara ya Masihi, aliiwtwa pepo mchafu.

<sup>154</sup> Kamwe hakufanya hivyo kwa jamii nyingine, Mmataifa, kwa sababu alisulubiwa, akaufufuka tena, naye Petro akahubiri Ujumbe kwa nyumba ya Kornelio, na kadhalika. Sasa, kamwe Yesu hakufanya hivyo. Lakini kumbukeni, iliahidiwa, wala Mungu hawezি kuvunja Maneno Yake, kwamba ingetendeka kwa Mataifa katika wakati wa mwisho, nabii alisema, “Kutakuwako na siku ambayo haitakuwa, haiwezi kuitwa mchana wala usiku, lakini wakati wa jioni itakuwa Nuru.”

<sup>155</sup> Sasa, tumekuwa na siku. Jua huchomozaje? Mashariki. Jua lile lile huvuka mlalo na kutua magharibi, si jua lingine, jua lile lile. Na wakati lilipochomoza mashariki, liliwaangazia watu wa mashariki, Wasamaria na Wayahudi. Na wakati alipokuwa kule alitoa ishara Yake kuonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi.

<sup>156</sup> Sasa, tumekuwa na miaka elfu mbili ya siku yenyе utusitusi, kitu kama msituni au giza kidogo zaidi. Tumekuwa na miamsho mikuu, tukitembea katika nuru yenyе utusitusi tuliyо nayo. Tumekuwa na siku ambapo tungeweza kufanya madhehebu makubwa, kujenga makanisa makubwa, shule kuu, seminari. Hivyo tu, sawa. Lakini ni wakati wa jioni sasa, jua linatua.

<sup>157</sup> Ustaarabu umesafiri pamoja na jua. Ustaarabu wa kale sana ni mashariki. Uchina ndio ustaarabu wa kale kuliko wote. Nao ustaarabu umesafiri pamoja na jua. Tuko wapi sasa? Kwenye Pwani ya Magharibi. Kama tukienda mbele zaidi kidogo, tumerudi mashariki tena. Tuko katika wakati wa jioni. “Na itakuwa Nuru wakati wa jioni.” Ni kitu gani? Jua lile lile.

<sup>158</sup> Sasa, Mungu ni Mungu asiye na kikomo. Yeye hana kikomo, tunajua hilo. Na kama Yeye, baada ya miaka hiyo yote ya mafundisho ya kiakili, naye akamjia Myahudi na Msamaria kabla ya mwisho wa wakati wao, na kuwaonyesha ishara ya Masihi, asingekuwa ni Mungu ye ye yule kama akituacha sisi

Mataifa tuingie juu ya dhana ya kiakili. Yeye hana budi kufanya jambo lile lile kabisa, Naye aliahidi atafanya hivyo kwa kanisa la Mataifa.

<sup>159</sup> Sasa, kwa manufaa ya ndugu zangu makasisi, wapate kuwa na dhana, ufahamu, pengine dhahiri zaidi kidogo, labda, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu."

<sup>160</sup> Sasa, hebu tuangalie tu dakika moja. Na tafadhalini, kama nikisema jambo fulani hapa ambalo linapinga ka—kanisa fulani, ama kitu fulani, ama madhehebu fulani, silimaanishi kwa njia hi—hiyo, ninajaribu tu kutoa hoja.

<sup>161</sup> Mwangalieni Ibrahimu, yeye alikuwa ndiye baba wa mataifa yajayo, kupitia Uzao Wake wa Kifalme, ambao ulikuwa ni Kristo. Sasa, isingeweza kutukia, ile ahadi kamili, kwa Wayahudi, kwa sababu kupitia kwa Isaka ahadi yote ni kwa jamii ya Wayahudi, bali katika siku hizi za mwisho Yeye ameiahidia Ibrahimu na Uzao wake, ambao, Kristo alikuwa Mzao wake, Kanisa liko upande huu. Sasa, si kwa Ibrahimu pekee, bali Uzao wake. Bwana akipenda, kama nkipata saa moja ama mbili zaidi, ningetaka kuwafundisha, *Ibrahimu Na Uzao Wake Baada Yake*.

<sup>162</sup> Angalieni jinsi alivyomleta Ibrahimu kupitia hizo njia panda za kuhesabiwa haki, utakaso, ubatizo wa Roho Mtakatifu, jambo lile lile tu kama Yeye alivyoufanya hapa, hasa, akamweka kama mwana, na kabla tu Sodoma haijangamizwa.

<sup>163</sup> Sasa, kumbukeni, kuna matabaka matatu ya watu, daima, kama vile Myahudi, Mmataifa, na Msamaria, hao ni mwaminio, anayejifanya mwaminio na asiyeamini, kwa hiyo tu—tunaona jambo hilo. Na kila mkutano huleta hayo, kila umati huleta hayo, tunayo tu.

<sup>164</sup> Sasa, angalieni siku hiyo, Ibrahimu hakushuka kwenda Sodoma, bali Lutu alishuka kwenda Sodoma. Alikuwa angali ni mwaminio, kama lile kanisa la kawaida, mwaminio wa taratibu za dini, hata hivyo alikuwa ni mwaminio. Naye alikuwa huko chini Sodoma kwa sababu alifikiri angeweza kupata pesa za ziada ama kuwa maarufu zaidi kidogo. Nafikiri alifanyika meya wa hilo jiji ama kitu fulani huko chini. Naye mke wake alikuwa mwanachama wa vilabu vyote, na kadhalika huko chini, na ilikuwa ni vigumu kwake kuondoka.

<sup>165</sup> Lakini kabla tu ya jambo hilo kutukia, sasa, angalieni, kulikuwako, Ibrahimu, alikuwa ni Mteule, nasi sote tunajua ya kwamba Kristo anakuja kwa ajili ya Kanisa teule, ya kwamba Unyakuo ni masalia, tunajua hilo, uh, Kanisa teule, hao wengine watapitia kwenye Hukumu, bali Wateule wanaenda kwanza katika Unyakuo, kwa sababu hawawezi kuingia Hukumuni.

<sup>166</sup> Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi yuna Uzima wa Milele. Yeye ayasikiaye maneno Yangu na kumwamini Yeye

aliyenipeleka yuna Uzima wa Milele wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani.” Yohana Mtakatifu 5:24. Tuko ndani ya Kristo, tayari tumehukumiwa, Mungu alituhukumu kwa ajili ya imani yetu katika Mwanawewe, Kristo Yesu. Na kwa Roho Mtakatifu tunabatizwa katika Mwili huo na kuwa sehemu ya Kristo, Wateule, Kanisa teule.

<sup>167</sup> Ibrahimu aliwakilisha Kanisa teule, kama tu vile Kanisa teule la Uzao wake baada yake katika siku hii. Mnalifuata? Ibrahimu, si Ibrahimu pekee, bali Uzao wake baada yake. Naye alikuwa baba wa mataifa, ambayo sisi hapa leo, mimi ni Mwairishi, na wengine, labda, Mhindi, na wengine Mnorwe, na wengine ni wengineo. Mnaona? Sote tumeketi hapa, lakini kwa... Mungu amefanya kutoka kwa damu moja mataifa yote. Sisi sote ni mmoja katika Kristo, “Kwa kuwa kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja.” Hiyo ni kweli. Hilo ni Kanisa teule.

<sup>168</sup> Sasa, kuna kanisa ambalo haliyamini katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, huko nje Sodoma, wangali wanafanya mambo wanayofanya Sodoma: kamari, karata, milo ya supu, mambo ya kila namna, wanavaa kama walimwengu, wanatenda kama walimwengu, wangali wanajiita washiriki wa kanisa. Mnaona? Hilo ni kanisa la Sodoma. Sasa, kabla tu ya mwisho kuja...

<sup>169</sup> Sasa, kumbukeni, neno *kanisa* linamaanisha “walioitwa watoke,” kama waliotengwa, waliotengwa na kutokuamini, wakiamini kila Neno la Mungu.

<sup>170</sup> Basi angalieni kile Ibrahimu: Ibrahimu hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, haidhuru ilichukua muda gani. Loo, wakati—wakati Sara alipokuwa na umri wa miaka sitini na mitano naye Ibrahimu akiwa na sabini na mitano, alikuwa mgumba, mke alikuwa tasa, na hata hivyo, Mungu alimwambia atapata mtoto kwa mwanamke huyo, naye akaamini na kufanya mipango kwa ajili yake. Na miaka ishirini na mitano baadaye angali aliamini jambo lile lile, ingawa hakuna ushahidi, ilikuwa ikienda mbali zaidi wakati wote.

<sup>171</sup> Lakini Biblia ilisema ukae... Huenda ukaombewa, useme, “Sioni tofauti yoyote kwangu,” halafu unarudi nyuma. Unaona? Huo si Uzao wa Ibrahimu. Uzao wa Ibrahimu unapoishika ahadi hiyo, hakuna kitu kitakachoutikisa, utakaa papo hapo, haidhuru!

Ninaweza kumsikia Ibrahimu akisema, akiingia, anasema, “Sara.”

“Naam, Mpenzi.”

“Ndio kwanza ni—nikutane na Mungu huko nje.”

“Loo!”

“Alisema tutapata mtoto.”

<sup>172</sup> Ungeweza kuwazia mzee wa miaka sabini na mitano, mwanamke mkongwe wa miaka sitini na mitano, wakashuka kwenda kwa daktari na kufanya maandalizi kwa ajili ya mtoto mchanga? Daktari anasema, “Wao, jamaa mzee, maskini jamaa mzee, amerukwa na akili.” Mnaona? Loo, hivyo ndivyo kila mtu aliye wa kiroho, kila mtu anayempenda Mungu, wanachukuliwa kidogo *wamechanganyikiwa*, mwajua, kwa hiyo, “Mbona, huyo jamaa mzee, achaneni naye; hana madhara.”

<sup>173</sup> Vema, Mungu alimwambia Ibrahimu, “Ujitenge na hao, ondoka, achana na kutokuamini huko.”

<sup>174</sup> Samahani, akina dada, sina budi kutoa hoja hapa. Lakini labda baada ya mwezi wa kwanza, ama siku *kadhaa*, ninaweza kumsikia Ibrahimu akisema, “Vipi kuhusu . . . ?” Mnaona, sasa, kumbukeni, alikuwa amekoma hedhi kwa yapata miaka ishirini. Kwa hiyo kasema, “Unajisikiaje, kipenzi?”

“Hakuna tofauti.”

“Mungu abarikiwe, tutampata kwa vyovyote vile. Shona vijibuti, na vijiblanketi vyote, na kadhalika, tutampata kwa vyovyote vile.”

“Unajuaje?”

“Mungu alisema hivyo.” Hilo latosha. Mungu alisema hivyo. Unaona?

Vema, mwaka mmoja ukapita. “Vipi kuhusu hilo, Mpenzi?”

“Hakuna tofauti.”

“Utukufu kwa Mungu, utakuwa ni mwujiza mkubwa zaidi sasa kuliko ulivyokuwa hapo kwanza, tutampata kwa vyovyote vile.”

<sup>175</sup> Miaka ishirini na mitano ikapita, sasa huyu hapa, maskini nyanya, mnaona, naye Ibrahimu ni mzee na mwenye umri mkubwa, sasa, “Mpenzi, unajisikiaje sasa?”

“Hakuna tofauti, Mpenzi.”

“Utukufu kwa Mungu, tutampata kwa vyovyote vile.”

“Unajuaje?”

“Mungu alisema hivyo.”

Sasa, Uzao wa Ibrahimu unachukua msimamo ule ule: “Mungu alisema hivyo.”

<sup>176</sup> Ndipo unasema, “Vema, niliombewa, bali siamini mimi ni tofauti hata kidogo.” Huo si Uzao wa Ibrahimu. La, la, Uzao wa Ibrahimu huamini.

Sijali ni nini, madaktari hamsini wangeweza kusimama, waseme, “Utakufa.”

“La, endelea, Daktari.”

“Unajuaje?”

"Mungu alisema hivyo." Hilo latosha.

<sup>177</sup> Sasa, angalieni, alikuwa akingojea, miaka ilikuwa imepita, urembo ulikuwa umetoweka, naye mke alikuwa mkongwe, na mume alikuwa mzee, basi siku moja Ibrahim, angali anaendelea kujitenga, akiwakilisha Uzao wa Ibrahim siku hizi, uliotengwa na ulimwengu, ulioitwa utoke, ukawekwa kando. Hao ni Wakristo, Wakristo halisi waaminio, waliowekwa kando, walioitwa watoke. Sasa, Ibrahim, akiketi kule juu kilimani, mambo hayakuwa yakiendelea vizuri sana, hakuwa tajiri, ng'ombe walikuwa wakifa kwa njaa.

<sup>178</sup> Lutu alikuwa anaendelea vizuri, alikuwa huko chini Sodoma, meya wa mji na, loo, alikuwa, mke wake alikuwa ni mwanachama wa vilabu vyote, nao, binti zake walikuwa wanachama wa mashirika yote, na, jamani, ninawazia walikuwa tu kama Wasodoma. Kwa hiyo hao hapo, huko chini Sodoma.

<sup>179</sup> Kwa hiyo basi, siku moja, wakati Ibrahim, akiwa ameketi kwenye kivuli cha mwaloni, ambapo hema yake ilipigwa, aliwaona watu watatu wakija wakitembea. Kuna jambo fulani tu kuhusu Mkristo, unapomwona Kristo, unaweza kutambua. Aliwaangalia watu hao, naye akatoka mbio kwenda kuwalaki. Sasa, yeye hakufanya kama kafiri, kusema, "Mabwana wangu." Alisema, "Bwana wangu, njoo, keti chini ya mti upate kupumzika, nami nitachota maji kidogo, kisha nitaitawadha miguu Yako. Jistareheshe, nami nitaleta kipande cha mkate ule." Alitaka kuwaburudisha, kwa sababu ndani ya moyo wake aliamini kulikuwa na jambo fulani kuhusu hilo. Alikuwa akilitarajia, mnaona.

<sup>180</sup> Kwa hiyo wakaketi chini, nami ninaweza kumwona akirudi hemani, mpaka alipokutana, kwenye hema kuu, akasema, "Sara, pepeta unga kidogo." Kwa maneno mengine, "kanda mikate," mwajua.

<sup>181</sup> Na ni wangapi wanaojua kukanda mikate kulikuwa ni nini? Ninakumbuka mama yangu alikuwa na maskini kichungio kikubwa, pia alikuwa na maskini pipa kubwa la kale, tuliweka unga mle ndani. Naye alikuwa na kabari, angekwangua kabari hiyo moja kwa moja juu ya kile kichungio, mwajua, na kutikisa unga wote kupika ugali wa mahindi.

Na kwa hiyo, akaenda na kusema, "Kanda u—unga kidogo, ama, unga." Kisha kasema, "Oka keki mekon."

Ndipo akakimbia mionganoni mwa kundi, naye akaona ndama mdogo, na kumchinja, akampa huyo mtu, ama, akamchinja, na kumpa mtumishi amtengenze.

<sup>182</sup> Naye akarudi nje na kusimama mbele yao, akaleta nyama na kuiweka chini. Sasa, kumbukeni, walikula hiyo nyama, na kunywa maziwa, na kula mkate.

<sup>183</sup> Angalieni, basi alimlisha hicho Nani? Mungu. Huyo alikuwa ni Mungu, Ibrahimu alimwita Elohimu. Ninyi ndugu mnajua hilo. Elohimu ni Yeye Ajitoshelezaye kwa Yote, kama alivyoanza katika Mwanzo 1, Elohimu. Elohimu, yule MIMI NIKÓ aliye mkuu, katika mwili wa mwanadamu, akila nyama, akinywa maziwa, akila ugali wa mahindi, huku ameketi chini ya mti wenye kivuli, akiwa na mavumbi nguoni Mwake, Mtu wa kawaida tu. Lakini Ibrahimu alijua huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu.

<sup>184</sup> Wawili wao walismama na kushuka kwenda Sodoma. Walishuka huko chini kuhubiri, huko chini Sodoma. Loo, kama wewe ni wa kiroho labda utalipata. Mliona? Hao wawili walioshuka kule, hawakufanya miujiza yoyote, ila tu walipofushwa macho yao wasiuone mlango. Na kuhubiri Injili huypofusha macho ya wasioamini. Lakini kulikuwa na watu wawili walioshuka kwenda kule kuhubiri, kumtoa Lutu Sodoma.

<sup>185</sup> Angalieni siku hizi, si ni ajabu katika siku hizi za mwisho, kwamba kote katika wakati, kuitia wakati wa Uzao wa Ibrahimu, njia panda ya kanisa, tumekuwa na Moody, Sankey, Finney, Knox, Calvin, Spurgeon, Wesley, na kadhalika, lakini kamwe, pia tulikuwa na Billy Sunday, lakini kamwe hatujawahi kuwa, hapo awali, na Billy *Graham*.

<sup>186</sup> Angalia, yule Malaika alikuwa amebadilisha jina la Abramu likawa *Ibrahimu*, lililoendelezwa A-b-r-a-m-u, I-b—I-b-r-a-h-i-m-u, akimpa sehemu ya Jina Lake, Ibrahimu, Elohimu, kwa sababu alikuwa awe baba wa mataifa, pia.

<sup>187</sup> Wala kamwe kanisa la kielimu kote katika wakati, halijawahi kumpokea mjambe, ambaye amejulikana kimataifa hapo kabla, mwenye jina linaloishia kwa h-a-m. Mnaona mahali lilipo? Billy Graham mamboleo huko chini Sodoma, “Ondokeni kwake.” Hivyo ndivyo Billy Graham anavyopiga mayowe, “Ondokeni kwake, mwisho umekaribia.” G-r-a-h-a-m, kamwe katika historia ya kanisa, lakini ndilo hili. Mwangalieni Bwana wetu akilirejea.

<sup>188</sup> Halafu kulikuwa na Malaika mmoja aliyesimama, akabaki nyuma pamoja na Ibrahimu. Angalieni ni mwujiza wa namna gani Yeye alilipa hilo Kanisa teule. Alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema. Kwa nini hakumwita Abramu? Alisema, “Ibrahimu, yu wapi mkeo,” sio S-a-r-a-i, bali S-a-r-a, “yu wapi Sara, mkeo?”

<sup>189</sup> Naye akasema, “Yuko hemani nyuma Yako.” Biblia ilisema ya kwamba li—lile hema lilikuwa nyuma ya yule Malaika, ama, yule Mjumbe, Mjumbe ameketi pale akila nyama, akinywa maziwa. Kasema, “Yuko hemani nyuma Yako.”

Akasema, “Ibrahimu, Mimi,” loo, kiwakilishi nafsi, “Nitakuzuru kwenye muhula wa maisha, kama nilivyoukuahidi.”

<sup>190</sup> Sasa, ninazungumza tu na kusanyiko lililochanganyikana, nanyi wasichana, samahani, kama hili linawakera, bali ni kujenga hoja: Sasa, Biblia ilisema wote wawili walikuwa na umri mkubwa, kama mume na mke, ilikuwa imekoma kwa miaka mingi. Mnaona, walikuwa na umri wa miaka mia moja. Labda miaka ishirini hawakuwa kama mume na mke. Naye Sara, moyoni mwake, akacheka kifichifichi, akisema, “Mimi, mwanamke mkongwe, mwenye umri wa miaka mia moja, niweze kupata raha na bwana wangu,” mumewe, “tena? Mbona, isingewezekana, mambo hayo hayajakuwa kwetu kwa miaka na miaka na miaka. Ingewezekanaje?” Naye akacheka kimoyomoyo.

Ndipo yule Malaika akasema, “Kwa nini Sara akacheka, akisema ya kwamba mambo haya kweli hayangeweza kutimia?”

<sup>191</sup> Bwana wetu alisema nini? “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Ati nini? Nuru za jioni ziliahidiwa Mataifa. Mungu yeye yule aliyejidhihirisha Mwenyewe pale, katika mwili wa mwanadamu, kisha akatoweka katika dakika moja, Mungu yuyo huyo angejidhihirisha Mwenyewe katika watu, mwili wa kibinadamu, umbo la Roho Mtakatifu, watu wanaoamini, katika siku za mwisho kwenye Nuru ya jioni. Yesu alisema hivyo. Nini? Kwa Mataifa, Uzao wa Ibrahimu, ambao ulikuwa ni mataifa mengi.

<sup>192</sup> Walikuwa na ninii yao, Malaika alikuwa amefanya, ishara kwa—kwa kanisa la kimadhehebu, G-r-a-h-a-m, yeye anafanya ishara Yake. Hiyo ni kweli.

<sup>193</sup> Na sasa, Malaika wa Mungu ndani ya Kanisa, lilitoteuliwa, Malaika akija kutoka Mbinguni, Roho Mtakatifu, Mjumbe, kuthibitisha ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, yale aliyofanya wakati huo, anafanya sasa.

<sup>194</sup> Yesu alisema, “Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi.” Na kama uhai ulio katika tawi ukizaa tawi, litaleta uhai ule ulio katika huo mzabibu. Na, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, nyingi kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba.”

<sup>195</sup> Kanisa, la kiakili, lina mjumbe wao. Kanisa, la kimbunguni, lina Mjumbe Wake, Roho Mtakatifu, akifanya na kutenda ishara zile zile ambazo Yesu alifanya alipokuwa hapa duniani. Basi Nuru ya siku hizi ni nini? Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele.

<sup>196</sup> “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.” Basi kile alichokuwa jana, ndicho atakachokuwa leo. Alifanya nini? Kwa Wayahudi na Wasamaria, si kwa Mataifa; bali iliahidiwa wakati wa jioni kwa Uzao wa Ibrahimu, ingekuwa ni jambo lile lile.

<sup>197</sup> Sasa, ningeweza kuzungumza kwa saa nyingine moja, ama *kiasi fulani*, juu yake, lakini Neno moja kutoka Kwake litakuwa zaidi ya milioni kumi, mimi, ama mhudumu mwингine yejote, angeweza kusema. Sasa, tunajua hiyo ni kweli, hayo ni Maandiko, hiyo ndiyo ahadi. Lakini sasa, je, atafanya hivyo? Hilo ndilo swal: Je, Yeye atafanya hivyo?

<sup>198</sup> Na sisi ni kitu gani? Tuko katika wakati wa jioni. Tunaishi chini ya Nuru za jioni. Kumbukeni, jua lile lile linalochomoza mashariki ndilo jua lile lile linaloangazia magharibi. Na j-u-a lile lile linalochomoza *kule*, ndilo j-u-a lile lile linalotua *huku* chini. M-w-a-n-a yule yule aliyeonesha nuru juu ya *hilo*, ndiye M-w-a-n-a yule yule katika siku za mwisho kwa Wasamaria, na kwa Wayahudi waliokuwa wakimtzamia, na sasa kwa Mataifa, tunapomtzamia wakati wa jioni. Mungu na awarehemu.

<sup>199</sup> Ninajua inawabidi kuharakisha kwenda nyumbani, mpate chakula chenu cha jioni, kisha mrudi kanisani tena. Kumbukeni, yachunguzeni Maandiko, leteni makaratasi yenu mpate kuyaandika Maandiko ninayonukuu. Kama hayako sahihi, mna—mnawajibika kwa uchaji kuja kwangu na kuonyesha. Sitaki kuwa makosani, bali siko makosani maadamu Maandiko yanasema *ndivyo* na Mungu analithibitisha. Mtu anaweza kusema chochote anachotaka, huyo ni mwanadamu, bali Mungu anaponena, mtu yejote asithubutu kulitilia shaka. Ni kutengwa Milele na Uwepo Wake, milele.

<sup>200</sup> Sasa, tungeweza kufanya nini? Kama tunaweza kutambua na kuona kwamba Yesu angali hai... Mbona, sisi, leo, tunaenda kwenye ibada, tunajifanya kana kwamba tunaenda kwenye ibada ya mazishi badala ya... tu—tunaenda ku—kutoa heshima kwa wafu, badala ya kumwabudu na kumsifu Mshindi. Kristo alishinda mauti, alishinda kuzimu, alishinda kaburi, alishinda dhambi, akashinda maradhi. Tunamsifu Mshindi, si mtu aliyeufufuka maelfu ya miaka iliopita aliyeishi maisha mazuri, bali Kristo aliyeufufuka tena, na ni yeje yule jana, leo, na hata milele.

<sup>201</sup> Huenda nikawa na mhemuko kidogo lakini kama ungejisikia jinsi nilivyojisikia, ungekuwa na mhemuko pia, kwa sababu ninajisikia kubarikiwa sana wakati huu, maana ni—ninajua ya kwamba Yeye yu hai, na Maandiko ni ya kweli. Kwa sababu Yeye yu hai, unaweza kuishi pia. “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.”

<sup>202</sup> Basi, Bwana Yesu, njoo katikati yetu, ingia katika miili yetu, ingia ndani ya ndugu zangu wahudumu, ndani yangu, ndani yenu huko nje, na uje tu na tujisalimishe Kwako, na kisha Wewe utekeleze na kuonyesha ya kwamba Wewe ni Kristo aliye hai, Roho wa Mungu anayeishi mionganii mwetu, ambaye hutekeleza na kulitimiza Neno Lako, na kuthibitisha yale yaliyoahidiwa.

Na tuombe sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa.

<sup>203</sup> Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa Milele, na Mpaji wa kila karama njema na kamilifu, na ile Zawadi iliyio kamilifu sana, Bwana, tunayoweza kuwazia ilikuwa ni Zawadi uliyotupa Wewe, Mwana wa Mungu, na kwamba Yeye yu hai leo, milele, na amekuwa pamoja na Kanisa kote katika wakati huu wa huzuni.

<sup>204</sup> Na sasa kama tunavyoona katika siku hii, ya kwamba Nuru inaangaza wakati wa jioni juu ya watu wa magharibi, ikithibitisha ya kwamba Wewe hutimiza Neno Lako kikamilifu, nami naomba, Mungu, ya kwamba kila mwanamume na mwanamke hapa leo apate kumpokea, kumwamini Yeye. Wale wasiomjua kama Mwokozi wao, jalia wampokee sasa hivi, na kusema, "Bwana, saidia kutokuamini kwangu."

<sup>205</sup> Jalia wale ambao bado hawajajazwa na Roho kwa ajili ya utumishi, jalia waseme, "Naam," huyo, "naam" wa Milele, kwa Roho Mtakatifu mkuu.

<sup>206</sup> Nami nimesoma kutoka kwenye Neno Lako leo, Bwana, labda kwa kuwa sina elimu na nimepungukiwa, kamwe sistahili kutoa ama kuyatambulisha Maandiko, bali yale niliyopungukiwa nayo, Roho Mtakatifu na ayatimize katika thibitisho. Tujalie, Bwana. Jalia liwe rahisi sana watoto wadogo wataliona, wote wataamini.

<sup>207</sup> Jalia kwamba kila mtu hapa aliye mgonjwa, aweze kuona, na kutambua, na kusema, "Yesu, Bwana wetu, yu hai, nami ninamwamini Yeye kwa ajili ya uponyaji wangu." Nao madaktari wao, bila shaka, watawaambia mara moja, "Mmepata nafuu sana miilini." Ndipo ndani ya miyo yao watajua ya kwamba Yesu ameingia kuushughulikia huo ugonjwa, nao watapata afya. Tujalie, Bwana.

<sup>208</sup> Wabariki wahudumu hawa wa-walioketi huku nyuma kwenye jukwaa hili. Na hapana shaka ni wa makanisa mengi mbalimbali. Pia mbariki mchungaji wa kanisa hili, wabariki mashemasi wake, wadhamini wake, wabariki walei wote kila mahali.

<sup>209</sup> Na kote katika bonde hili na nyanda hizi pana, tuma uamsho katika kila kanisa, tuma uamsho kwa Waanglikana, na kwa Wapresbiteri, na kwa Wapentekoste, na kwa wote, Bwana, ili kwamba kuwe na kutembelewa kukuu kwa Roho Mtakatifu wa Mungu hapa katika Grande Prairie, kwamba habari zitaenea kote mikoani, na kote katika mataifa, na milki, ya kwamba Yesu angali hai.

<sup>210</sup> Tunatamani kumwona, Bwana. Na kama vile ndugu yetu alivyosema vizuri asubuhi ya leo, aliposema, akija, alikuwa amefanya, akifuata vibao vya kuelekeza, akiangalia kile kibao, apitie wapi ili kuja Grande Prairie, si hicho kibao kilichomleta hapa, kibao ndicho kilichomwelekeza hapa. Kwa hiyo na watambue leo, kama vile nimeyanukuu Maandiko,

“Sisi tunataka kumwona Yesu,” jalia kila mtu hapa aweze kukuona Wewe, Bwana, katika nguvu za kufufuka Kwako, ukiishi mionganoni mwetu.

<sup>211</sup> Na tutakapoondoka alasiri ya leo, kama nilivyonukuu hapo awali, jalia twende nyumbani kama wale waliotoka Emau. Walitembea pamoja Nawe siku nzima, Wewe ulizungumza nao, ukawaelezea Maandiko, bali hawakutambua ilikuwa ni Wewe, ndipo jioni hiyo, ulipofanya kana kwamba ungepita, nao waka—wakakusihii kwamba uingie na kukaa pamoja nao, Ee Mungu, jalia wanafunzi leo, kama Kleopa, wakusihii uje ukae pamoja nasi, Bwana. Nawe ulipoingia mahali pao padogo pa nyumba ndogo ya wageni, Nawe ukafunga milango, na halafu ukafanya jambo kama ulivyofanya kabla ya kusulubiwa, ndipo macho yao yakafumbuliwa, kwa kuwa walijua kwamba hakuna mtu aliyefanya hivyo kabisa.

<sup>212</sup> Baba, sisi ni wahudumu, na makasisi, na wajumbe wa agano, bali hatuwezi kulifanya hivyo, Bwana. Hatuwezi kufanya mambo uliyofanya Wewe, bali Wewe unaweza kuja na kulitimiza Neno Lako kwamba—kwamba kazi ulizofanya, sisi pia tungezifanya.

<sup>213</sup> Basi njoo, Bwana Yesu, na ufanye mambo kama uliyofanya kabla hujasulubiwa, kusudi hawa Wakristo, watu wanaomcha Mungu wapate hakikisho ya kwamba Bwana wetu hajafa, bali amefufuka tena, na jalia, kama Kleopa na rafiki yake, waende nyumba hadi nyumba wakisema, “Hakika, Bwana amefufuka,” wepesi na wachangamfu, si kubishania dini yao, bali kusema, “Bwana amefufuka.” Tujalie, Baba.

<sup>214</sup> Tunajikabidhi, miili yetu, roho zetu, na yote yалиyo ndani yetu, tunayakabidhi Kwako sasa, tukingojea kusikia Neno moja tu kutoka Kwako, Nalo litatosha, Baba. Kama utathibitisha tu ya kwamba unaishi hapa mionganoni mwao, basi watakuamini, Bwana, watu hawa wenye mioyo minyofu, watu wa uwandani, watakuamini Wewe, kisha wataenda nyumbani, haitawabidi kusema, “Ndugu Branham alifanya *hivi na vile*,” kwa sababu wanajua nisingeweza, bali watasema, “Bwana wangu yu hai, nami nampenda, nami nitamwabudu, nami nitahudhuria kanisa Lake, nami nitaninii, ni—nitatimiza wajibu wangu kama Mkristo, nitashuhudia, nitamwamini Yeye siku zote za maisha yangu.” Hilo ndilo kusudi tunaloombea, katika Jina la Yesu. Amina.

<sup>215</sup> Mnampenda? Ninyi Wamethodisti wote mnampenda? Wabaptisti, Wapresbiteri, Wapentekoste, wote mnampenda? Hebu tuimbe kifungu kimoja kidogo tu. Ninapenda kumwabudu baada ya kukatakata katika Neno na kadhalika. Hebu tumwabudu tu kwa wimbo pamoja na wimbo huo mzuri wa kale wa kanisa, *Nampenda*. Ni wangapi wanaoujua? “Nampenda, kwani...” Hebu tuuimbe.

<sup>216</sup> Na hebu tuache... Usiangalie ni nani anayeketi karibu nawe, usijaribu kuwa na... Chochote nisichokipenda, ni sauti iliyofunzwa kupita kiasi, wakishikilia sauti yao mpaka uso wao ni wa samawati, hawaimbi, wanapiga tu makelele. Lakini ninapenda uimbaji mzuri, wa mtindo wa kale, wa moyoni, ambapo huenda usiweze kuibeba tuni kwenye ndoo, lakini hata hivyo, unaimba kutoka moyoni mwako. Sasa, unasema, "Vema, mimi si mwimbaji." Hilo halijalishi. Mfanyieni Bwana kelele za shangwe, basi. Maandiko yanasema hivyo.

Nampenda, nampenda  
 Kwani alinipenda kwanza  
 Na kununua wokovu wangu  
 Mtini Kalvari.

<sup>217</sup> Sasa, tunapouimba tena, peaneni mikono, ninyi, ninyi nyote wa madhehebu mbalimbali na mbalimbali, peaneni mikono, mseme, "Mungu akubariki, nina furaha kuwa hapa katika ibada." Ninajaribu, kufanya nini? Kumfanya Roho wa Mungu atende kazi mionganii mwenu. Mnaona?

Nampenda (...?...)  
 Mtini Kalvari.

<sup>218</sup> Sasa, mnajua kile tunachopaswa kufanya? Paulo alisema, "Nikiabudu, nitaabudu katika Roho; nikiimba, ninaimba katika Roho." Kwa hiyo na tuyafanye yote mawili pamoja, tunapoinua mikono yetu na kufunga macho yetu, kwa upole na utamu sana katika Roho:

Nampenda (...?...)  
 Kwani alinipenda kwanza  
 Na kununua wokovu wangu  
 Mtini...

Sasa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu na kuuvumisha.

Sasa, piano inaucheza, huku sisi miyoni mwetu tukiabudu.

<sup>219</sup> Ee Yesu, Mwana wa Mungu, Ua la Uwandani, Nyinyoro ya Bondeni, Nyota ya Asubuhi, tuko katika uchache, Bwana, ikija kwenye idadi ya ulimwengu, lakini kama Maandiko yasemavyo, tunaye Yesu.

<sup>220</sup> Hatujaribu kushindana na ulimwengu katika mazoezi yao muhimu sana ya kisaikolojia. Hatujaribu kumetameta kuwashinda kwa michezo ya mpira na burudani za kiakili, hatuwezi kukutana nao, Baba, ulisema, "Watoto wa usiku wana hekima kuliko wa mchana." Kwa hiyo tunajua hilo, Baba, bali tunaye Yesu, hawana Huyo.

<sup>221</sup> Na kama mtu huyo yuko hapa, leo, asiye na Yesu, na kujua ya kwamba wamepita kutoka mautini kuingia Uzimani, jalia hii iwe ndiyo saa ambayo watampokea sasa, kama Mwokozi wao, wajazwe na Roho Wake, kwa kuwa tunaomba, katika Jina Lake, na kwa ajili ya utukufu Wake, tunaomba. Amina.

Na (...?...)  
 Kwani alinipenda kwanza . . .

Si mnaupenda tu huo?

Loo, ni ushirika ulioje, loo, ni furaha iliyoje ya  
 Kiungu,  
 Kuegemea kwenye mikono ya milele;  
 Nina amani kamilifu pamoja na Bwana wangu  
 aliye karibu sana,  
 Kuegemea tu kwenye mikono Yake ya milele.

Sasa, ninyi ni wazuri sana, kusanyiko zuri sana, ndivyo  
 livilyo, ninajua Mungu atawafanyia jambo fulani.

<sup>222</sup> Sasa, ndiyo kwanza nimwulize mwanangu, kwa kawaida tunasambaza kadi kila siku. Kadi haikupi hakikisho la chochote. Ni kushikilia tu kadi tupate . . . nitawaonyesha katika kusanyiko hili dogo. Ni wangapi hapa wanaotaka kuombewa, uwе na kadi au la? Inua mkono wako. Kote tu kwenye kusa- . . . , sasa, ni nani atakayetangulia? Haya basi. Mnaona? Inakubidi kuwa na njia fulani ya kuwapanga mstarini.

<sup>223</sup> Sasa, mnaona, mimi . . . Herufi gani? A. A, moja hadi hamsini. Vema. A, namba moja hadi namba hamsini ndipo tutakapoanza kuwaombea wagonjwa. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Simjui huyo mvulana. Sijawahi kumwona. Nitampa kisogo, kama nilivyozungumza nanyi kuhusu jambo hilo alasiri ya leo.

<sup>224</sup> Bwana, sikujuji. Kama hatufahamiani, inua mkono wako. Wala sijawahi kukuona maishani mwangu, si zaidi ya vile ulivyopanda hapa juu. Sasa, nimekupa kisogo.

<sup>225</sup> Lakini ili kuwaacha watu, kusanyiko lione (kama atafanya hivyo) ya kwamba Yeye anatimiza ahadi Yake: Kama alivyokuja katika mwili wakati huo, na kujidhihirisha Mwenyewe kwa Ibrahim, Yeye anaingia katika mwili wake ambao ameukomboa, na kujidhihirisha Mwenyewe kwa Uzao wa Ibrahim. Mnaelewa hilo?

Sasa, Mungu wa Mbinguni anajua, simjui huyu mtu.

<sup>226</sup> Sasa, ninachukua kila . . . Huyu hapa, Yeye yupo hapa sasa. Ninachukua kila roho chini ya . . . hapa ndani, chini ya mamlaka yangu katika Jina la Yesu Kristo. Nguzo hiyo ya Moto mnayoionna kwenye hiyo picha, Yeye hayuko futi mbili kutoka mahali ninaposimama sasa.

<sup>227</sup> Sasa, hebu mtu aliye nyuma yangu, aombe tu, aseme, “Bwana,” ama chochote kilicho shida, huenda akawa mgonjwa, huenda akawa na matatizo ya kifedha, si—sijui. Chochote kile, jalia Roho Mtakatifu athibitishe Neno la Mungu papa hapa mbele zako.

<sup>228</sup> Sasa, Mungu wa Mbinguni, liko mikononi Mwako, mikononi Mwako, mimi ni mtumishi Wako tu. Na jalia ijulikane ya kwamba Wewe ni Mungu nami ninautangaza Ujumbe Wako kwa kweli na kwa usafi. Nimekuheshimu Wewe, Bwana, sasa, liheshimu Neno ambalo nimehubiri. Ninajikabidhi Kwako katika Jina la Yesu Kristo, ili watu hawa wapate kujua ya kwamba Wewe ni Mungu na mimi ni nabii Wako.

<sup>229</sup> Mtu anayesimama nyuma yangu hajiombei mwenyewe, anamwombea mtu mwininge, na huyo ni mtoto, mtoto huyo hayupo hapa. Mtoto huyo anaugua henia. Kama utaamini kwa moyo wako wote, hiyo henia itamwacha mtoto huyo. Je, mambo hayo ni kweli? Kama ni kweli, inua mkono wako. Basi nenda ukaamini na upokee ulichoomba.

<sup>230</sup> Ninataka kuzungumza na wewe, wewe ni mwanamke. Yesu alikutana na mwanamke kisimani wakati mmoja. Hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana, nadhani, maishani, hatufahamiani. Hii... Wewe ni mdogo sana wa umri kuliko mimi, na labda tulizaliwa umbali wa maili nyingi, tumeachana kwa miaka mingi, na hii hapa mara yetu ya kwanza kukutana. Sasa, Yesu alikutana na mwanamke wakati mmoja, mimi si Yeye, wala wewe siye yule mwanamke, bali ili Neno Lake lipate kutimizwa, kuwafanya watu waone ya kwamba—ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele...

Mtu fulani kwenye kusanyiko, jambo fulani lilitukia kwenye kusanyiko. Inanibidi tu kulifuatilia, ni... Ninaiona ile Nuru, ni ono, linatoka tu.

<sup>231</sup> Sikujui wewe, kama nilivyosema. Naye Yesu alikutana na mwanamke katika mandhari ndogo kama *hii*, Naye akazungumza naye dakika chache apate kujua siri ya moyo wake, ndipo akamwambia shida yake ilikuwa ni nini. Naye akasema, upesi, “Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii. Tunajua ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo haya.”

Yesu akasema, “Mimi ninayenena Ndiye.”

<sup>232</sup> Ndipo akakimbia mjini na kusema, “Njoni, mwone Mtu Ambaye ameniambia shida ni nini,” yale mambo aliyofanya. Kasema, “Je, haimkini huyo kuwa ndiye Masihi?”

<sup>233</sup> Sasa, mama, alasiri ya leo, mimi sikujui, wewe hunijui, ama, mimi, basi kama Roho Mtakatifu anadumu ye ye yule, aliyekuwa ndani ya Yesu, yuko ndani yetu, kwa sababu Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake, mnaona, Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu, nasi ni wana na binti za Mungu walipewa mamlaka, na kama Yeye ataniambia jambo fulani ambalo umefanya, jambo ulilopanga kufanya, jambo lililokuleta hapa, ugonjwa fulani, ama—ama mtu fulani unayetaka aombewe, ama kitu fulani, kinge kufanya uamini na kuwa na imani?

Je, wasikilizaji wengine wangeamini? Unamjua mwanamke huyo, mtu yejote? Vema.

<sup>234</sup> Sasa, usiogope. Wewe ni Mkristo, maana ninahisi mtetemo wako wa roho yako. Unaona? Wewe ni Mkristo mwaminio, huna chochote cha kuhofia. Kuwa tu mnyenyekuvu, amini. Jambo moja unalouguu ni ugonjwa wa fadhaa, una fadhaa kupindukia. Hiyo ni kweli. Nawe una shida ya kike, ugonjwa wa akina mama, tezi zilizoshuka. Hiyo ni kweli.

<sup>235</sup> Sikubahatisha hilo. Nilikuwa nikijaribu kutafuta mahali hilo linatoka. Sikubahatisha hilo, hilo si kubahatisha, huo ni ukweli. Hiyo ni kweli, mama? Inua mkono wako.

<sup>236</sup> Hebu nione, hata sijui yale niliyosema, njia pekee nitakayojua, ni kuishika hiyo kanda. Huo ni upako, uko katika ulimwengu mwagine, kiwango kingine.

<sup>237</sup> Naam, huyu hapa anakuja, ninamwona, has...huo ni ugonjwa wa fadhaa, yeye anaugua huo, hasa sana jioni wakati amechoka sana, anakuwa mchovu sana basi. Na, naam, ninaona uchunguzi unaonyesha alikuwa na shida ya—ya wanawake. Hiyo ni kweli. Yeye pia, ana u—ugonjwa wa kibofu nyongo, pia ana ugonjwa wa moyo, ni moyo wenye wasiwasi. Mambo hayo ni kweli, sivyo? Hiyo ni kweli.

<sup>238</sup> Mtu mwagine unataka aponywe pia, sivyo? Ni mume wako, aliyeketi papa hapa nje. Unaamini Mungu anaweza kuniambia ana shida gani? Kama nitafanya hivyo, unafikiri angeukubali kama uponyaji wake? Ungefanya hivyo? Ndipo ugonjwa wa pumu utamwacha. Hakika, unaamini. Nenda, amini sasa. Usiwe na shaka, Yesu Kristo atakuponya. Mungu akubariki.

Unaamini kwa moyo wako wote sasa? Amini tu, usiwe na shaka.

U hali gani?

<sup>239</sup> Huko nyuma kabisa, upande wa nyuma, akitketi kule nyuma, huyo mama anayeugua mawe ya nyongo. Ulikuacha basi, mama, kwa hiyo unawenza kwenda na kuwa mzima. Yesu Kristo anakuponya.

<sup>240</sup> Sikujui wewe, hatufahamiani. Kama Mungu atanielezea shida yako ni nini, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake, na kuamini ya kwamba Yeye yu hai? Ninataka kukuambia jambo hili, una—unajua kwamba jambo fulani linaendelea, hisia tamu sana, nyenyekuvu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako ili kusanyiko liweze kuuona.

<sup>241</sup> Ninaangalia moja kwa moja kwenye Nuru hii. Kama ninyi ndugu hapa mnaweza kuona, angalieni kati yangu na yeye, mnaona Nuru hiyo yenyre rangi ya zumaridi, ikisonga? Sasa, hapa, mwanamke huyo ananiondokea.

<sup>242</sup> Naam, ana uvimbe, na uvimbe huo uko upande wa kushoto, karibu na titi, chini ya titi la kushoto. Hiyo ni BWANA ASEMA

HIVI. Mwamini Yeye kwa moyo wako wote, unaweza kuponywa. Una imani? Unaamini kwa moyo wako wote? Usiwe na shaka sasa, amini tu, useme, "Ninaamini."

<sup>243</sup> Unaumwa na kichwa, sivyo? Una kadi ya maombi? Naam. Huihitaji tena. Sikuju. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Uligusa nini?

<sup>244</sup> Nawaulizeni, aligusa nini? Yuko futi ishirini kutoka kwangu, ama thelathini. Kamwe hakunigusa, bali alimgusa yule Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wake. Hiyo ndiyo sababu anaweza kuponywa, kwa sababu anaamini. Ninakupa changamoto kuliamini. Angalia kinachotukia.

<sup>245</sup> Huyu ndiye yule mama, yule...? U hali gani, mama? Hatufahamiani, pia, nadhani. Mungu anatujua sote wawili, hiyo ni kweli? Unaamini ya kwamba Mungu anatujua sote wawili?

Unazungumza nini, Kinorwe? Njoo hapa. Mtu ye yote ambaye ni Mjerumani? Yuko wapi yule ndugu Mjerumani? Unazungumza Kijerumani? Naam?

Hivi hatufahamiani? (La, mwa—mwambie, katika Kijerumani, unaona.) Sikuju.

<sup>246</sup> Naam...?...Naam, bwana. Hilo ni sawa. Hebu kidogo. Sasa, angalia hilo ono. Je, unaweza kusema, "ono"? Kama nikiona ono, mwambie, shida yake, ili aamini. Kama mimi...? Yeye anataka—yeye anataka—yeye...?...Yeye ni Mje-...? Unazungumza Kijerumani? Vema. Hebu kidogo. Naam. Unaona, jinsi hili ono lilivyo. Sasa, huna budi kulishika upesi sana, maana linaniacha. Sasa, wewe sema tu yale ninayosema. Unaona? Kwa hiyo ataninii... Liseme katika Kijerumani.

<sup>247</sup> Kama Mungu atanifunulia kile kilichokuleta hapa, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Kama ndivyo, inua mkono wako. Unaugua...(Ninalishika sasa, ngoja mpaka nitakapolipata tena. Unaona? Huh? Hebu tulishike linapokuja, maana inanibidi kulisema jinsi tu ninavyoliona. Alikuwa... Nilikuwa papo hapo, lakini hilo ono likaniacha kwa dakika moja tu.) Ana ugonjwa wa tumbo na unasababishwa na ugonjwa wa wasiwas. Ugonjwa wa wasiwas husababisha ugonjwa wa tumbo. (Liseme sasa.) Ningejuaje hilo wakati hata siwezi kuzungumza lugha yako mwenyewe? Mungu hunifunulia.

Kuna kitu fulani moyoni mwako. Unataka mtu mwininge aombewe, ni mume wako, uko masikioni mwake, hayupo hapa, lakini kama utaamini!

Sasa, ye ye anaelewa Kiingereza!

Sasa, unaweza kwenda ukaupokee katika Jina la Yesu, na upate kile unachoomba.

<sup>248</sup> Sasa, vipi kuhusu hilo? Mnaona, wakati tafsiri ya Kiungu ilipokuja, alilingia kwenye mkondo. Ingekuja... Nilifikiri labda ingekuja, ili uweze kuona kwamba Mungu angeweza kukufanya

uelewe lughu yoyote unayotaka. Na wakati nilipokuwa katika lile ono, bila kujua nilichokuwa nikizungumza, alielewa katika Kiingereza wakati huo. Mnaona? Hilo hapo, ninii... Loo, Yeye si ni halisi? Sasa, huyo ni Bwana wetu Yesu, Ambaye ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

<sup>249</sup> Weka tu mkono wako juu ya wangu. Unaamini kwa moyo wako wote? Basi kisukari kitakuacha, nawe unaweza kwenda nyumbani, uwe mzima. Naam, uh-huh. Mwaminini Mungu.

<sup>250</sup> Ulipokuwa umesimama pale, ukinizungumzia, umekuwa ukilemaa kwa yabisi kavu, ilikuwa vigumu kwako kuamka asubuhi. Nimekuwa na wakati mgumu, hilo ndilo lililonifanya, katikati ya hilo ono, ulikuwa na imani nydingi sana, ulikuwa ukiivuta kutoka kwa mwanamke huyo wakati wote. Hiyo yabisi kavu umekuwa nayo, isahau, endelea, utakuwa mzima na utapata afya. Mungu anakuponya.

Vema, mgongo uko sawa sasa, unaweza kwenda nyumbani, uwe mzima. Yesu Kristo anakuponya.

Sasa, hivi hukujisikia vizuri sana niliposema jambo hilo? Kwa sababu ulikuwa na kitu kile kile, nawe uliponywa wakati uo huo.

Hebu tuseme, “Mungu asifiwe, atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu.”

Na jambo lile lile tena. Aisee! Ugonjwa wa mgongo! Bwana asifiwe. Nenda ukaamini, kwa moyo wako wote.

<sup>251</sup> Sasa, unaugua ugonjwa wa wasiwasi wakati huu. Kila mtu, wanajaribu, kukwambia, “Jirudie,” lakini huwezi, kuna kitu kinachokutisha na kukutia wasiwasi. Sisomi mawazo yako, bali usingeweza kuyaficha maisha yako hata ufanye nini, unaona. Lakini umekuwa ukijaribu kupata mahali ambapo ungeweza kuanzia, useme, “Kutoka papa *hapa*, nitaanzia, kutoka *hapa*.” Hiyo ni kweli? Uko mahali hapo sasa hivi. Mwamini Bwana Yesu Kristo, wasiwasi utakuacha. Nenda, na uwe mzima katika Jina la Yesu Kristo.

<sup>252</sup> Unakabiliwa na upasuaji kutokana na uvimbe. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuponya huo uvimbe, auondoe begani mwako, na kukufanya mzima? Kwenye bega lako la kushoto. Nenda na uamini, nao utakuacha.

Hebu tuseme, “Bwana asifiwe.”

Yabisi kavu. Unaamini kwa moyo wako wote atakupa afya na kukuponya? Nenda, ukimwamini Mungu, naye Mungu atakujalia.

<sup>253</sup> Sasa, ulipokuja hapa muda mfupi uliopita, nami ikanibidi kukuuta, ulikuwa umechoka kidogo. Sikutaka uwe mchovu, kwa sababu mtu aliye na ugonjwa wa moyo hapaswi kuchoka kamwe, bali huna tena sasa, Yesu anakuponya, kwa hiyo nenda zako tu.

Mnaamini huko nje kwa moyo wenu wote?

<sup>254</sup> Vipi kuhusu yule mama anayeketi hapa mwenye mishipa iliyovimba, akiniangalia? Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, mama? Unaukubali? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Liamini. Mwamini Mungu.

<sup>255</sup> Mama aliyeketi kule nyuma akiwa na ugonjwa wa mguu, unaamini Mungu atakiponya hicho kiungo, akupe afya? Kama unaamini, likubali tu na useme, “Mungu na ashukuriwe,” unaweza kuupokea.

<sup>256</sup> Ninampa changamoto kila mmoja wenu katika Jina la Yesu Kristo, kuamini ya kwamba huyo ni Mungu akionyesha ishara kwamba Yeye angali ni Masihi. Ni yeze yule jana, leo, na hata milele. Unaamini hilo? Inueni mikono yenu.

<sup>257</sup> Sasa, nitawanukulia Neno Lake. Hivi ndivyo alivyosema... Sasa, Yeye yupo, siwezi kufanya mambo hayo. Ninadhoofika, ninawaona tu kwa shida sasa, mnaona, kwa sababu linafifia tu. Ikiwa moja la hayo...

<sup>258</sup> Mwanamke aligusa vazi Lake na ni kitu gani kilichotukia? Vipi...? Unafikiri lingefanya nini, Yeye Mwana wa Mungu, na mimi mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema? Danieli aliona ono moja, akafadhaika kichwani mwake kwa siku nyingi. Hiyo ni kweli, ndugu? Na inakufikisha mahali ambapo... Nami ni dhaifu, kwa vyovytote vile, kutokana na kuendelea kwa miezi sita.

<sup>259</sup> Sasa, Yeye yupo hapa. Kristo wa Mungu yupo hapa. Kuna mmoja hapa ambaye hajakuwa mwaminio mpaka wakati huu, wangetaka kuinua mikono yao na kusema, “Ndugu Branham, niombee, sasa ninamwamini Bwana Yesu Kristo kwa moyo wangu wote na kumkubali kama Mwokozi wangu”? Mungu akubariki, huko nyuma, mama. Kunawenza kuwa na mwingine? Mungu awabariki. Mungu akubariki, bwana. Mungu awabariki, huko nyuma. Kupitia kwenye marefu ya katikati?

<sup>260</sup> “Mimi sasa, katika Uwepo wa Kristo aliyefufuka, Ambaye nitasimama mbele Zake kwenye Siku ya Hukumu!” Kumbuka, utasimama mbele za Roho yeze yule aliye hapa sasa, kwenye Siku ya Hukumu, kutoa hesabu kwa yale uliyofanya alasiri ya leo. Utampokea? Utampokea?

<sup>261</sup> Mtu yeze kwenye marefu haya ya kushoto hapa chini? Inua tu mkono wako, useme, “Nimekuwa mfuasi wa kanisa. Kwa kweli sijawahi kuzaliwa mara ya pili, sijui maana ya kuwa Mkristo aliyewekwa wakfu kabisa, lakini sasa ninayaweka wakfu maisha yangu Kwake. Ninataka kuwa Mkristo, wakati Uwepo Wake upo hapa, na anajua.”

<sup>262</sup> Unasema, “Ni nini...Ninajuaje?” Mwajua? Huyo Ndiye anayezungumza nawe, sasa hivi moyoni mwako. Kwamba... 

61-0516A Yesu Kristo Yeye  
Yule Jana, Leo, Na Hata Milele  
Zion Gospel Tabernacle  
Grande Prairie, Alberta Canada

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)